

# Mkombozi Aye Jamaa Wa Karibu

Jeffersonville, Indiana, USA

Oktoba 02, 1960

1 Asante, Ndugu Neville. Bwana akubariki. Ni vizuri sana kurudi tena, asubuhi ya leo, kurudi katika nyumba ya Bwana. Ninaamini ilisemwa, wakati mmoja, "Nilifurahi waliponiambia, 'Na twende nyumbani mwa Bwana.'"

Charlie, njoo huku nyuma ya nguzo hiyo, na uje hapa na kujipatia kiti. Njoo huku juu. Dada, je! Kuna kiti kule nyuma, mahali fulani, tungeweza kujisukumiza? Hapa pana mahali papa *hapa* juu, mama. Njoo papa hapa juu. Hapa, Charlie, njoo hapa na uketi karibu na Banks hapa juu, kwa hiyo haitakubidi kusimama. Kila wakati mvulana huyo anapokuja kutoka huko chini mbali sana Kentucky, akifika hapa, yeye husimama, kila asubuhi. Nasi tutamleta moja kwa moja hapa.

2 Hapa pana mahali hapa, kwenye mwisho wa kiti hapa, kwa ajili ya mtu mwingine. [Ndugu Neville anasema, "Kuna mama hapa, pia." — Mh.] Kuna mama anayesimama huko nyuma, huko nyuma. Njoo moja kwa moja hapa. Hapa kuna kiti papa hapa, dada, karibu kabisa. Njoo moja kwa moja mbele. Nami nadhani mtu fulani yuko kwenye kiti cha magurudumu pale. Sivyoy? [Dada fulani anasema, "Ndugu Branham?"] Naam. ["Kuna kiti papa hapa."] Kuna kiti kingine papa *hapa*. Ikiwa mtu anataka kimoja, nyuma huko nyuma, papa hapa pana kiti papa hapa. [Ndugu fulani anasema, "Na hapa kuna kimoja, Ndugu Branham."] Hiki hapa kimoja papa hapa juu, pia, jistareheshe. ["Kingine, hapa."] Naam. Unaweza kupata kimoja papa hapa. Sasa, njoni huku, ketini. Na ninajisikia tu halisi ...

Tunataka mstarehe wakati tukijaribu kuleta Neno la Bwana. Loo, hakika ni vizuri kuwa hapa.

3 Sijamwona Charlie jukwaani. Je, yuko huko nyuma? Vema, mleteni hapa. Jamani! Nimekuwa na Charlie, kule chini, siku chache zilizopita, wala siwezi kupita bila kwenda nyumbani kwake na kula, kwa hivyo nitamleta jukwaani, asubuhi ya leo. Kila siku akija hapa, husimama karibu na ukuta pale, kumpa mtu kiti. Kwa hivyo niliangalia huko nje asubuhi ya leo na kumwona amesimama pale, nikawazia, "Nita—Nitamleta humu ndani sasa." Vema, ni—ni sawa. Sasa tutapata ujumbe asubuhi ya leo kutoka kwa Ndugu Russell Cox. [Ndugu Branham na kusanyiko wanacheka — Mh.] Yuko wapi Nellie? Mimi ... Hiyo itakuwa safari nzuri kwake. Wapi? Naam. Jambo ndilo hilo.

4 Vema, hakika nina furaha kuona wengi wa marafiki huku. Jumapili iliyopita nilipoondoka, nilijisikia vibaya wiki nzima. Nilikuwa na rafiki mzuri aliyeketi hapa, kutoka huko chini kabisa Kusini, Ndugu West. Na nilikuwa nimezunguka, kupitia kwenye kusanyiko, nimechelewa. Nikasema, "Nina furaha kumwona *Fulani na Fulani*," nami nikamruka Ndugu West, wala kamwe—kamwe sikumtambua hata alipoanza kutoka nje. Ndipo nikawazia, wiki nzima, "Ndugu West atadhani si—sikunjali makusudi." Lakini yeye ni—yeye ni Mkristo, kwa hivyo anajua bora kuliko hayo. Anajua kuwa mimi...rafiki wa kweli. Nami najua anajua, nisingefanya hivyo.

5 Nilikuwa nikifikiria asubuhi ya leo, nikishuka kuja, kuwaona watu ambao wametoka sehemu mbalimbali. Sasa, huyu hapa Ndugu West hapa tena, asubuhi ya leo. Na Ndugu na Dada Kidd hapa, kutoka Ohio. Na baadhi ya ninii wangu...

Ninajua Ndugu Evans yupo hapa. Nilienda kumwona, jana alasiri, kwenye moteli, lakini nadhani alikuwa ametoka pamoja na Ndugu Fred na hao wengine. Nao wanakuja kutoka huko mbali Macon, Georgia, hapa, kila Jumapili ninapohubiri. Kutoka Macon, Georgia, hiyo ni mbali sana huko chini. Ni kama maili mia nane, au zaidi, nadhani, huko chini. Kuendesha gari pamoja na familia yake, kila siku ninapohubiri. Na huo ni uaminifu.

6 Nami nilikuwa—nilikuwa nikiwazia, loo, basi, kama una marafiki kama hao, wanaotaka kusimama na wewe! Sasa, hiyo...hao watu hawatoki huko mbali Georgia, na Ohio, na sehemu mbalimbali za taifa, kuja kwenye maskani hii ndogo hapa, kunisikia mimi. Wanakuja hapa kwa sababu wanaamini Ujumbe huo. Hivyo ndivyo wanavyoamini. Wanaamini Ujumbe huo. Basi ninapaswa kuwa mwaminifu na mkweli juu ya Ujumbe huo jinsi gani! Kwa sababu, sio—sio tu kwamba mimi, ninakosea, lakini ninamwongoza mtu mwingine vibaya. Mnaona? Ndipo basi Mungu ataniwajibisha kwa kosa lao, kwa sababu mimi ndiye niliyefundisha hilo. Mnaona?

Nami nawaambia, hakika inakufanya ufikirie kindani unapowazia mambo kama hayo. Kwa hivyo na—nathamini kila mmoja wenu, ni vizuri sana kujua kwamba ungeendesha gari hayo mamia ya maili, kupitia barabara zenye hatari na juu ya barabara hizi kuu, ambapo ajali na kadhalika. Imani yenu katika Mungu huwaongoza, kwa namna fulani, inawaleta hapa na kuwarudisha. Tuna furaha sana kuwa na marafiki wa aina hiyo. Ninaomba baraka nyingi za Mungu ziwe juu yenu.

7 Sasa, Jumapili iliyopita, ni—nilisema, "Vema, tutazungumza, halafu nitaita tu mstari wa maombi." Nimekuwa nikijaribu kufanya kazi kwa njia fulani, kujaribu kutafuta njia ya kuwaombea watu wengi zaidi. Na kama nikiwapitisha wengi zaidi kama Jumapili iliyopita, mimi...mtu fulani atakuwa akiniombea. Niliondoka hapa, karibu saa nane. Wala si—sikusambaza kadi za maombi.

Kusambaza kadi za maombi ni kazi ngumu. Sijui kama mnajua hivyo, au la, watu wanakuchukia. Naye Ndugu Banks Wood, alisema, hivi majuzi, tulipokuwa huko Kentucky, kwamba angejitolea na kusambaza kadi za maombi ikiwa Billy hakuvingia. Kwa hivyo Billy, kwa kuwa ni mwanangu, mwajua, mbona, wao... Mimi hupata barua chache, "Aliniahidi kadi ya maombi na hakunipa. Maskini mtundu huyo!" Kwa hiyo wao ... Hawezi kuzisambazia kila mtu. Wala hatuwezi kuwaweka wengi kupita kiasi mstarini! Mnaona? Hana budi kunilinda.

8 Basi—basi tulipotoka, binti-mkwe wangu alisema, "Bill, itabidi umrudishe Billy huko nyuma na kadi za maombi, au," kasema, "hutadumu sana."

Na, kwa hivyo, lakini ambapo nilifanyia kosa, ilikuwa ni kuanza utambuzi, kisha mtu fulani akarudi, kasema, "Nilisahau, mama alitaka kuombewa." Mnajua sababu ya kurudi kwao, ni kwa ajili ya utambuzi huo, mnaona. Kwa hivyo, lakini, siwalaumu. Ningefanya jambo lile lile. Mnaona? Ningefanya ninii ... Sisi ni wanadamu, na sote tunataka kuishi, na tunataka kujua la kufanya. Ndivyo tulivyo... Lakini unaweza tu kwenda umbali huo na mambo hayo, wewe, ya karama, ndipo basi karibu umekwisha, wakati mara kadhaa hilo linapotukia.

Na kwa hivyo Ndugu Banks alikuwa asambaze kadi za maombi asubuhi ya leo, ndipo ikatokea kwamba Billy aliingia jana usiku. Kwa hivyo nilifikiri hilo lingekuwa baya sana, kumwacha mtu mwenye sifa nzuri, mambo kama Ndugu Wood, kuzisambaza kadi za maombi, kufanya watu wamwingilie. Nadhani Billy hajali. Yeye amezishikilia kwa muda mrefu sana, kwa hiyo anaachilia tu. Vema.

9 Sasa—sasa wiki hii ijayo ninapaswa kuwa Dallas, Ijumaa hii ijayo usiku, kwenye mkutano wa Sauti ya Uponyaji. Ikiwa kuna watu wowote karibu na hapo, ninapaswa kuwa huko usiku huo mmoja, kuzungumza katika mkutano wao. Nami ninataka kuzungumza juu ya somo la *Njia ya Kuuendea Ushirika*, Bwana akipenda.

Na halafu, labda, labda Jumapili inayofuata, hiyo itakuwa Jumapili hii ijayo, Bwana akipenda. Sasa sina hakika sana. Bwana akipenda, Ninataka kurudi na kuzungumza juu ya somo ambalo nilipaswa kuzungumzia leo hii, *Upepo Katika Kimbunga*. Nami nilikuwa niwaombe wagonjwa, leo. Na hiyo kwa namna fulani ni kemeo kali kwa—kwa kanisa kwa ajili ya dhambi zake. Na—na hilo si somo zuri sana kuzungumzia wakati unapoenda kuitisha mstari wa maombi. Unapaswa kujenga imani ya watu kwa...kwa maombi, na kwa Mungu, na kuwa na imani. Kwa hivyo nilimwambia Ndugu Neville atangaze kwamba nitazungumza asubuhi hii juu ya somo lingine, kujenga imani katika watu, kwa Mungu. Kwa maneno mengine, kuwakemea watu kwa—kwa kutozishika amri za Mungu. Kwa njia hii, inawajenga watu huku, kuwa na imani katika Mungu. Mnaona?

10 Na nyuma katika chumba cha maombi asubuhi ya leo, au chumba cha kurekodia kule nyuma, maskini rafiki yangu wa zamani, Ndugu Kidd, themanini na, umri wa miaka themanini, anayeketi hapa. Wengi wenu mnakumbuka nilipomkimbililia hivi majuzi asubuhi, alikuwa—alikuwa karibu...imekuwa karibu mwaka mmoja uliopita, karibu nao sasa. Akifa, mahututi sana, nao madaktari wakampa wiki moja ya kuishi. Au, sio wiki, wao... Asingeweza kuishi kufikia asubuhi apate kuletwa huku chini, karibu asubuhi tatu zilizopita. Na sasa alikuwa ameshuka hadi mia moja na tano, au kitu kama hicho. Alisema, dakika chache zilizopita, amerudi kwenye mia na thelathini na mbili. Alisema alijisikia kama mvulana.

Ndugu Kidd, nashangaa ikiwa ungeweza kusimama tu, watu wapate kujua mhubiri huyu mzee ni nani. Huyu hapo. Hebu tuseme, "Asante Bwana." [Kusanyiko linasema, "Asante Bwana!" — Mh.] Mtu akifa kwa kansa, katika hali hiyo—katika hali hiyo. Yeye ana rafiki mdogo wa kupendeza pale. Laiti angalisimama, pia. Ninaninii tu ... Dada Kidd, vipi kuhusu wewe kwenda kule juu? Sasa, yeye ... Mnaona jinsi anavyoweza kuamka haraka? Haraka kuliko ninavyoweza. Mungu awabariki Ndugu na Dada Kidd. Jalia baraka nyingi za Mungu zikae juu ya ... Asante, dada.

11 Wanajitahidi kupitia milima ya Kentucky, juu chini kwenye njia za eneo la makaa ya mawe, wanafukuzwa, wanatupwa nje, na kudhihakiwa, wanateswa, wanaishi kwa chochote wawezacho. Wanasaga mahindi ambayo wangepata njiani, mahali fulani, na kuuishia Ufalme wa Mungu. Na umri wa miaka themanini, wakihubiri Injili, bado. Sasa, wamezeeka sana hawawezi kutoka nje, kwa hivyo mimi huomba vitambaa vya maombi na kuwatumia, na wao wa—wanaendelea tu kuvipeleka hospitalini na vitu kama hivyo. Watu huja na kuvichukua. Sasa, huko kweli ni kuwa nalo moyoni. Sivyo? [Kusanyiko linasema, "Amina." — Mh.] Ikiwa huwezi kwenda huko nje kukutana nao, unaweza kuwatumia kitambaa cha maombi, namna hiyo, watu wakiwa na imani. Hilo ni zuri sana.

12 Ndugu Rogers ameingia, pia, mahali fulani humu ndani leo, baba mkwe wa Ndugu Creech, rafiki yangu mpendwa sana. Huenda nyumbani kwake kama vile tu ninavyoshuka kwenda kwa Charlie na kwa Nellie na huko chini sasa, na kule Kentucky. Basi—basi nilikuwa nikienda kule chini na kuwinda, wakati wote, pamoja naye. Na hapa, si muda mrefu uliopita, yapata miezi kumi na mitatu iliyopita, daktari alimfanyia upasuaji. "Akiwa na saratani, na," akasema, "amekwisha."

Nami nikawaza, "Rafiki yangu wa thamani!" Askari mkongwe, Vita vya Kwanza vya Dunia, mtu shujaa

kweli, familia yake. Nami nilimbatiza katika Jina la Yesu Kristo, miaka mingi iliyopita, kwa ondoleo la dhambi yake, nikijua basi kwamba aliwekwa katika Mwili wa Kristo, naye alikuwa tayari kwenda kumlaki Mungu. Nikawaza, "Ndugu yangu mpendwa atasonga mbele sasa." Ilikuwa ni mara baada ya ono hilo, ama kabla ya ono hilo kunijia mimi, kuhusu Mbinguni. Ndipo nikashuka nikaenda kumwona, na chumbani ukaja upinde wa mvua. Mungu akayabadilisha mambo. Hiyo imekuwa miezi kumi na mitatu iliyopita, na bado yuko hapa leo, akila.

13 Alimeza aina fulani, akameza aina fulani ya vidonge vya salfa, vikamchoma kooni mwake *hapa*. Naye atakuwa katika mstari wa maombi, nadhani, asubuhi ya leo, ujao. Nami najua kwamba ninatangaza hilo Billy akiisha kuzisambaza, au akienda kuzisambaza, walijua ya kwamba watasambaza kadi za maombi. Nilimwambia mkwewe, rafiki yangu mzuri, Ndugu Creech, amlete—amlete huku. Ndipo nikawazia, kama nikimkosa, basi nitamkamata na kumweka katika moja ya vyumba hivi vya maombi hapa. Lakini alikuwa na kadi ya maombi. Nami nikasema, "Busty, nataka uende huko nje." Jina lake ni Everett. Tunamwita tu Busty, kwa kifupi. Naye—yeye ... Nikamwambia, "Nenda zako uingie kwenye mstari wa maombi. Afadhali nikuombe wakati upako ukiendelea, kwa ajili ya jambo hilo." Kwa hiyo ninapenda kuwa na ... Ikiwa najua nilikuwa nikiombewa, ninataka mtu awe na upako wakati wakiniombea.

14 Sasa hebu na tufungue Biblia yetu, asubuhi ya leo, tufungue Kitabu cha Ruthu. Nitasoma Maandiko kutoka kwenye hiki, kutoka kwenye Kitabu cha Ruthu. Na sasa kabla tu hatujaliendea somo hili ... Kama ningependa, ningetaka kutangaza somo langu la asubuhi ya leo, linaitwa: *Mkombozi Aliye Jamaa wa Karibu*. Nami ningetaka kuliendea kutoka kwenye misimamo minne mbalimbali, juu ya ukombozi.

Nikiwaza, Jumapili iliyopita, ilikuwa nikihubiri jinsi ambavyo Kristo alikuja kutukombo. Na halafu, leo, ninataka kuzungumza juu ya: Mkombozi ni nini? Anakuwaje Mkombozi? Basi, kumbukeni, Mkombozi anakukombo kabisa, wakati Yeye anapokukombo; kutoka kwa dhambi zako, kutoka kwa ugonjwa wako, kutoka kwa kila kitu kilicho kibaya. Yeye ni Mkombozi.

Sasa, kabla hatujaliendea, hebu na tuinamishe vichwa vyetu na kuzungumza Naye, kwa maombi. Na sasa huku vichwa vyetu vimeinamishwa, sijui ni wangapi asubuhi ya leo, katika Uwepo, wangetaka kukumbukwa katika maombi, kwa kuinua mikono yenu na kusema, "Mungu, unaona ... unajua haja yangu?" Mungu akubariki, kila mmoja.

15 Baba yetu wa Mbinguni, nina furaha sana, leo, ya kwamba kuna Nguvu kuu zilizo kuu, tukijua ya kwamba, Mungu, ya kwamba tunaweza kumkaribia kupitia Mwanawe, Kristo Yesu, na kuwa na—na jibu kwa yale tunayoomba. Kama ilivyokuwa katika mkutano uliopita, tulikuwa tukizungumza juu ya jinsi ambavyo watu walitangatanga huku na huku katika ngozi ya kondoo na ngozi ya mbuzi, na walikuwa ukiwa, wakitafuta Mji ambao mwenye kuubuni na kuujenga alikuwa ni Mungu. Wakijua laiti wangaliweza kamwe kumwenda mara moja, laiti wangeweza kupata mahali alipokuwa! Kama Ayubu, wa kale, alivyosema, "Laiti ningeweza kwenda, niubishe mlango Wake," kwa maneno mengine. "Laiti ningeweza kupata mahali Yeye—Yeye anapokaa, ningenda Nyumbani pamoja Naye, na ninge—ningeongea Naye, ana kwa ana." Lakini hapakuwa na njia kwa mwanadamu kufanya jambo hilo, kwa sababu alikuwa ametenda dhambi, na alikuwa amejitenga na kuwa mgeni kwa Mungu.

Bali kupitia kwa Yule wa thamani ambaye alikuja na kufungua njia, na kutosamehe dhambi zetu, na kutuleta mbele za Mungu, si kama wageni, bali kama watoto wanaomjia Baba yao. Tukijua ya kwamba Yeye atatupa kila ombi tunaloomba. Sheria moja tu ndiyo iliyowekwa, hiyo ni kusema, "Kama unaweza kuamini." Hayo ndiyo makubaliano. Shetani anadai ya kwamba hatutaamini, na Mungu anasema tutaamini. Sasa vita vinaendelea, na uamuzi ni wetu wa kufanya. Vyovyote uamuzi wetu utakavyofanywa, hivyo ndivyo itakavyokuwa. Na imeandikwa vizuri sana, "Mambo yote yanawezekana kwa hao waaminio."

16 Nasi tunaamini, leo, tunakuja, tukikukaribia Wewe tupate kibali cha Kiungu, tukiomba kwamba Wewe utayazingatia maombi yetu. Na kila mkono ulioinuliwa, Wewe unajua chini ya mkono huo, moyoni mwao, yaliyomaanishwa. Kwa maana imeandikwa, kwamba, "Wewe unajua makusudi na mawazo ya nia, na unaweza kuitambua nia." Nasi tunaomba, Mungu, ya kwamba utajibu kulingana na utajiri Wako na neema Yako, kwa kila haja ambayo ilitajwa.

Tungeomba pia leo, Bwana, kwamba utanisaidia, anayehitajika zaidi, labda, wa hili kusanyiko; nikijua kwamba, waliowekwa mbele zangu hapa, ni wale walionunuliwa kwa Damu ya Bwana Yesu. Kuna, labda, wenye dhambi walioketi hapa, ambao wamefungwa sana na dhambi, hata ingekuwa vigumu kwao, karibu, haiwezekani, kwao kufikia mahali pa kumkubali Kristo, mradi tu Shetani amewafunga sana kwa nguvu zake. Lakini tukijua ya kwamba imeandikwa, "Katika Jina Langu watatoa pepo."

17 Na utupe nguvu leo, Bwana, kwa kuhubiriwa kwa Neno, kumtoa kila pepo wa mashaka na ushirikina na hofu, kutoka mioyoni mwa watu na nia zao. Ili wale ambao wamefungwa na vurugu na mashaka wapate kuletwa mikononi mwa Kristo. Na pia imeandikwa, ya kwamba, "Wataweka mikono yao juu ya wagonjwa nao watapata afya." Kuna wale hapa ambao ni Wakristo, na wamefungwa na pepo wa magonjwa.

Bwana, nipe nguvu leo, za Roho Mtakatifu, kumkomboa kila mtu mgonjwa na anayeteseka aliye hapa jengoni leo, ili Roho Mtakatifu mkuu apate kuwa na ukuu katika kila moyo na kila mtu aliye katika Uwepo wa Kiungu.

Nena nasi kupitia Neno Lako. Neno Lako ni Kweli. Bila kujua tu la kusema, bali kungojea uongozi wa Roho Mtakatifu, apate kutuongoza na kutuongoza katika Kweli yote. Tujalie, Bwana. Jipatie utukufu. Na umtie mafuta mtumishi Wako. Na Neno Lako tayari limetiwa mafuta. Tutakupa sifa, wakati ukilipeleka kwenye kila moyo, kama tulivyo na haja. Katika Jina la Yesu Kristo, tunaomba, Mwana wa Mungu. Amina.

18 Kabla ya kusoma, huenda nikasema kauli mbiu hii ndogo ninayoipenda sana.

Kama una mito ambayo huwezi kuivuka,  
Na una milima usiyoweza kupitia,  
Kumbuka tu, Mungu Mbinguni ni mtaalamu  
Katika mambo wasiyoweza kufanya wengine.

Ninasoma kutoka Kitabu cha Ruthu, mlango wa 1.

*Ikawa zamani za Waamuzi walipoamua, ... kulikuwa na njaa katika nchi. Akaondoka mtu mmoja wa Beth-lehemu ya Yuda, akaenda kukaa katika nchi ya Moabu, yeye, na mkewe, na wanawe wawili.*

*Na jina la mtu huyo aliitwa Elimeleki, na ... mkewe Naomi, ... majina ya wanawe ... Maloni na Kilioni, Waefrathi wa Beth-lehemu ya Yuda. Wakafika katika nchi ya Moabu, wakakaa huko.*

*Akafa Elimeleki, mumewe Naomi; ... yule mwanamke akasalia, na wanawe wawili.*

*Nao wakaoa wake katika wanawake wa Moabu; na jina la ... mmoja aliitwa Orpa, ... jina la wa pili Ruthu: wakakaa huko yapata miaka kumi.*

*... Wakafa na Maloni na Kilioni wote wawili; na hao wanawake wakafiwa ... huyo mwanamke akawa amefiwa na wanawe wawili, na mumewe pia.*

*Ndipo alipoondoka, yeye na mkwewe, ili kurudi kutoka nchi ya Moabu: maana yeye ... amesikia katika ... amesikia ya kwamba BWANA amewajilia watu wake na kuwapa chakula.*

*Basi akatoka pale alipokuwapo, na wakweze wawili pamoja naye; wakashika njia ili warudi mpaka nchi ya Yuda.*

*Kisha Naomi akawaambia wakweze wawili, Nendeni sasa mkarejee kila mmoja nyumbani kwa mamaye: BWANA na awatendee mema nanyi, kama ninyi mlivyowatendee mema hao waliofariki na mimi pia.*

*BWANA na awajalie kuona raha kila mmoja nyumbani kwa mumewe. Kisha akawabusu; nao wakapaza sauti zao wakalia.*

*Wakamwambia, La, sivyo, lakini tutarudi pamoja nawe kwa watu wako.*

*Naye Naomi akasema, Enyi wanangu, mrejee: kwa nini ninyi kufuatana na mimi? Je, mimi ninao watoto wa kiume tena tumboni mwangu, hata mweze ... hata ... wawe mume wenu?*

*Enyi wanangu, mrejee, nendeni zenu; kwa kuwa mimi ni mzee siwezi kupata mume tena. Kama ningesema, Natumaini, kama ningempata mume hata usiku huu, na kuzaa watoto wa kiume;*

*Je, mngesubiri hata watakapokuwa watu wazima? Mngewangojea ... kwa ajili yao ... mngejizua msiwe na waume? La, sivyo, wanangu; maana ninaona chungu sana kwa ajili yenu, kwa sababu mkono wa BWANA umetoka juu yangu.*

*Nao wakapaza sauti zao, wakalia tena: na Orpa akambusu mkwewe; lakini Ruthu akaambatana naye.*

*Akasema, Tazama, shemeji yako amerudi kwa watu wake, na kwa mungu wake: basi urejee wewe umfuate shemeji yako.*

*Naye Ruthu akasema, Usinisihi nikuache, nirejee nisifuatane nawe: maana wewe uendako nitakwenda; na wewe ukaapo, nitakaa: watu wako watakuwa watu wangu, ... Mungu wako atakuwa Mungu wangu:*

*Pale utakapokufa, nitakufa nami, na papo hapo nitazikwa: BWANA anitendee hivyo na kuzidi, ila kufa tu kutatutenga mimi na ... wewe nami.*

19 Ninataka kuyaita mazungumzo haya madogo asubuhi ya leo, ninapoyafundisha, nikijaribu kuleta imani kwenu, ya ukombozi, na kwamba ni nini, na jinsi ya kuupokea. Ninataka kuyaita: *Mkombozi Aliye Jamaa Wa Karibu*.

Sasa, *kukomboa chochote*, ni "kukirudisha." Kitu ambacho kimepotea, kama vile kuweka kwenye duka la rehani. Nawe unashuka uende kukikomboa hicho, kinakombolewa kwa gharama. Ndipo ni mali yako ya kibinafsi, ukiisha kukikomboa. Lakini sheria ya ukombozi, katika Israeli, ilibidi awe ni jamaa wa karibu, kuikomboa mali au kitu fulani kilichokuwa kimepotea.

20 Hadithi yetu inaanzia katika wakati wa watawala wa Israeli, ambao walikuwa ni waamuzi, baada ya kifo cha Yoshua. Na kupata picha nzuri sana ya jambo hili, soma kuhusu sura tano au sita za kwanza za Samweli wa Kwanza, nawe uta—utapata hadithi yake halisi.

Lakini tutaruka sasa tupate muktadha mkuu wa jambo hili. Ambapo, wakati fulani uliopita, nilianza kwenye Kitabu hiki cha Ruthu, nami ilinichukua wiki tatu au nne, nikikipitia. Niliaza kwenye Kitabu cha Ufunuo, siku moja, na ikanichukua mwaka mzima, karibu, kukipitia. Kila Andiko dogo linaungana moja kwa moja na lingine, kabisa, kote katika Biblia. Inapendeza. Kwa hiyo, tunajua Biblia imevuviwa. Kwa kuwa, kimahesabu na kwa kila njia, hakuna fasihi nyingine iliyoandikwa ambayo haitajipinga mahali fulani.

Kitabu hiki kiliandikwa kwa kipindi cha karibu miaka elfu nne, Vitabu vya Biblia. Navyo viliandikwa na baadhi... Ninasahau ni watu wangapi walioviandika. Nilikumbuka. Lakini, samahani. Ninataka kusema sitini na kitu, lakini mimi—mimi ni—mimi ni... Huenda nikakosea pale. [Ndugu fulani anasema, "Arobaini." — Mh.] Arobaini. Watu arobaini waliandika Biblia, katika kipindi cha maelfu ya miaka, bila kujuana, wala kuonana, au kusoma baada ya mwingine, mara nyingi. Na hakuna neno moja linalopingana na lingine. Imevuviwa!

21 Sasa, watu wengi wanaangalia Kitabu hiki cha Ruthu, kama wasemavyo, "Ni hadithi ya mapenzi ya Biblia." Biblia ni hadithi ya mapenzi. Biblia nzima ni hadithi ya mapenzi.

Sio tu kwamba ni hadithi ya mapenzi, bali ni nabii. Si kwamba ni nabii tu, bali pia ni historia. Sio kwamba tu ni ha—hadithi ya mapenzi, historia, nabii, ni Mungu Mwenyewe. Kwa sababu, "Hapo mwanzo kulikuwako Neno, naye Neno alikuwako kwa Mungu, naye Neno alikuwa Mungu." Kwa hiyo, Neno ni Mungu katika maandishi. Hilo linapaswa kulitatu, ndugu; Mungu katika maandishi. Yehova, akichapishwa kwenye Kitabu. Na hakuna hata moja ya hayo ni namna fulani tu ya hadithi ya kubuni, bali yote ni Kweli kabisa. Kila sehemu Yake, iweke nafsi yako. Iko Hapo. Ni Ukweli, na Mungu atalitetea Neno Lake.

22 Na hadithi hii iliandikwa, na hati zote za kale. Wakati walipokuwa wakiitenganisha Biblia, wale watu watakatifu, wakati walipokuwa wakijaribu kuiweka pamoja katika Agano la Kale, Kitabu hiki cha Ruthu kilikuwa kimoja cha Vitabu bora sana ambavyo walivikubali. Kwa nini? Ikiwa ni hadithi tu ya mapenzi, kwa nini waandishi na wahenga wa kale wakubali Kitabu hiki kuwa kimevuviwa? Kwa sababu, kuna ufunuo uliofichwa ndani Yake. Na katika ufunuo huu uliofichwa, unapata maana halisi. Utakuleta karibu sana na Mungu.

Nami naomba, nafsi yangu yote, asubuhi ya leo, kwamba Mungu ataushika kila moyo, auduwaze kabisa, hata ajifunue Mwenyewe, kile tu alichu, katika hadithi hii; kile Yeye alichu kwako; jinsi ya kumkubali. Na mara ukiliona, ni rahisi sana, unashangaa jinsi gani ulivyopata kupita juu yake. Lakini inaweza tu kufunuliwa na Roho Mtakatifu.

23 Sasa, wengi, wanapoisoma Biblia, wanaisoma, wanasimama tu na kusoma ukurasa, na kusoma ukurasa. Kamwe hutaipata. Kwa sababu, iko katika vitendawili. Naye Yesu alimshukuru Mungu kwa kuifanya namna hiyo. Kasema, "Umeificha kutoka kwa macho ya wenye busara na wenye akili, na utaifunua kwa watoto watakaojifunza."

Kama ambavyo nimesema mara nyingi. Mke wa Branham anayeketi kule nyuma, asubuhi ya leo. Lakini ninapokuwa ng'ambo, yeye ataniandikia barua. Yeye atasema, "Mpenzi Bill, nimeketi hapa, usiku wa leo, pamoja na watoto. Ninakuwazia." Ndipo anaendelea na kuandika kile atakachoandika. Lakini ni—ninampenda, nami ninamjua vizuri sana, ninaweza kusoma katikati ya mistari. Ninajua hasa yale anayosema, mnaona, ikiwa atayaandika hapa au la. Mnaona? Maana, ninajua yale anayosema. Kwa nini iwe hivyo? Hayo ni mawasiliano ya karibu. Sisi ni mmoja. Mnaona? Naye anajua tabia yangu, ninajua yake. Yeye haninii ...

Anaweza tu kuketi na kuniangalia. Ninaweza kuwaambia yale atakayosema, mnaona, kwa sababu ni—ninamjua vizuri hivyo. Naye anaweza kunifanya vivyo hivyo. Sasa, ni nini kinachofanya hivyo, ni kuaminiana. Upendo!

24 Jana asubuhi, tulikuwa tumelala kitandani tumechelewa kidogo, na watoto hawakulazimika kwenda shuleni, nasi tukaanza kuzungumza juu ya mambo mbalimbali. Na jinsi ... "Chuki ilikuwa nini?"

Nikasema, "Chuki ilikuwa na mwanzo, kwa hiyo haina budi kuwa na mwisho. Upendo haukuwa na mwanzo, kwa hiyo hauna mwisho. Chuki ni ya enzi na enzi. Upendo ni wa Milele. Chuki huanza na chuki

itaisha. Upendo haukuanza kamwe wala hautakwisha." Mnaona? Ulikuwa ni wa Milele.

Na wakati mwanamume anapompenda mwanamke na kumwoa kwa sababu yeye ni mrembo tu, kutakuwa na mwisho kwa hilo. Lakini wakati mwanamume anapompata mwanamke anayempenda, hajui ni kwa nini, bali anampenda. Naye anampata mwanamume anayempenda, haidhuru anaonekanaje. Mwanamume anampenda mwanamke. Mwanamke anampenda. Huyu ni mwenzi wa Milele Utukufuni. Wata — ... Mauti wala kitu kingine cho chote kinachoweza kuwatenganisha, kwa sababu wametoka kwenye Umilele. Nao wakatoka nje, katika kipindi cha wakati, nao watarudi kwenye Umilele. Umilele umeshuka chini katika mwili, unaiotwa wakati, kisha unarudi moja kwa moja kwenye Umilele tena. Hauwezi kuangamia.

25 Mwanamke ambaye ni mrembo, urembo huo utafifia, hakika tu. Hebu upe miaka michache. Labda, leo, anajinyonganyonga mtaani, maskini mwanamke fulani nusu uchi, akizipeleka nafsi nyingi kuzimu kuliko vilabu vyote vya pombe nchini. Lakini atajinyonganyonga mtaani, akifikiria yeye ni kitu. Kama vile Biblia ilivyosema, "Wangukuwa na shingo zilizonyoshwa, kutamanisha, *hatua za madaha*," (hiyo inamaanisha kujinyonganyonga) "wanapotembea," katika siku za mwisho. Wakitimiza Maandiko, wala hawajui. Wanasimama uani, wamevaa nguo chafu, wanaume wakimwangalia, wala hajui. Huenda akawa mwadilifu, kwa mumewe ama mpenzi wake mvulana, kadri awezavyo kuwa; lakini, kwenye Siku ya Hukumu, yeye atajibu kwa kufanya uzinzi na mamia ya wanaume. Kuna roho juu yao, nao hawajui. Biblia ilisema, "Uchi, kipofu, wala hujui." Sehemu ya kusikitisha ni, "Hujui."

Lakini je, ulijua, maskini umbo hilo lililolumbika, ambalo Mungu amempa msichana huyo, huenda likawa limeoza kwenye wakati huu Jumapili ijayo? Mtu huyo mrefu, mweusi na mwenye sura nzuri huenda asiwe kitu ila tu lundo la takataka, ifikapo Jumapili ijayo. Hayo yote yanaangamia.

Lakini kile kilicho ndani, Mungu, upendo, huishi Milele. Kwa hiyo, angalia ndani. Weka macho yako kwenye lengo.

26 Sasa, hadithi hii inaanza kitu cha namna hiyo, kama mwanamke anayependeka, mzuri. Jina lake lilikuwa Naomi. *Naomi* maana yake ni "mwenye kupendeza." *Elimeleki* alikuwa ni mumewe, maana yake ni "kuabudu." "Ibada ya kupendeza" ilikuwa ni familia yake. Walikuwa na mtoto wa kiume, *Maloni*, ambalo linamaanisha "ugonjwa." Na *Kilioni*, yule mwingine, alimaanisha "kuchoka, huzuni, majonzi." Hiyo hapo hiyo familia.

Ndipo kukaja njaa katika nchi ya Israeli. Na kosa la kwanza ambalo Myahudi amewahi kufanya, ni kuondoka katika nchi hiyo. Mungu aliwapa nchi hiyo. Wakati Ibrahimu alipopewa hiyo nchi, Mungu alimwambia asiondoke katika nchi hiyo. Naye alifanya kosa aliposhuka akaenda Gerari, akapata shida. Myahudi hapaswi kamwe kuondoka Palestina. Hapo ndipo alipopangiwa.

27 Nao wamefukuzwa, kote ulimwenguni. Na sasa wanarudi tena. Loo, ni hadithi nzuri sana tuliyo nayo hapa, asubuhi ya leo. Wanarudi.

Naomi alitoka kwa sababu ya njaa, Naomi na Elimeleki, nao wakaenda Moabu.

Sasa kupata msingi wa hadithi, kwa hiyo, unaposikiliza, utaweza kufahamu ni nini.

Sasa, Wamoabu- ... Wamoabu, walitoka kwa mwana haramu, ambaye alikuwa ni binti za Lutu. Baada ya kuutoroka moto wa Sodoma, kwa neema ya Mungu, basi hao mabinti walimlewesha baba na kuishi naye, kama mke. Wakazaa mtoto. Ndipo mmoja wao alianzisha, na akaleta ta—taifa la Moabu, likidhaniwa kuwa Wakristo, lakini walikuwa wamechanganyana na upagani. Na, mnaona, kuiacha nchi ya ahadi, haidhuru ilikuwa mbaya jinsi gani, kuwa mgeni katika nchi nyingine, kulileta shida.

28 Na wakati wo wote ambapo mwaminio anaondoka kwenye ardhi aliyopewa na Mungu! Mara nyingi, katika siasa, uchaguzi huu unaokuja na kadhalika, mtu mzuri anaweza kuwa mtu mzuri, naye atatangatanga atoke kwenye misingi hiyo. Kama vile mhudumu fulani ninayemjua, aligombea umeya wa jiji. Basi alipogombea umeya, akatoka katika misingi yake ya huduma, ndipo Shetani akampata.

Kama Mkristo ye yote akiondoka kwenye misingi hiyo. "Vema, nitashuka tu, usiku wa leo, nikaketi pamoja na wavulana kwenye chumba cha karata, kwa muda kidogo. Sitafanya madhara yoyote. Nitakunywa tu kinywaji kimoja kidogo." Uko nje ya misingi yako. Rudi. Unajitia tu hatarini.

"Loo, hao wasichana wengine wote huvuta sigara. Nitajaribu moja tu." Uko nje ya misingi yako. Usifanye hivyo. Kaeni katika nchi ya uenyeweji wenu. Usifanye, "Kweli, kila mtu hapa, wananiita, 'Mzee mpumbavu.' Wananiita, 'Mtindo wa kale.'" Kaa hapo, hata hivyo. Hapo ndipo mahali pako. Dumuni ndani ya Kristo.

29 Naomi, kwa sababu ya njaa, alitangatanga kutoka nchi hizo na akaingia Moabu, akitafuta chakula. Haikumlazimu kufanya hivyo, kwa sababu hao wengine walikaa katika Uyahudi, Bethlehemu. Bethlehemu maana yake, Betheli, "nyumba ya Mungu," nyumba ya sifa. Nao walikaa humo.

Naye akatangatanga pamoja na mumewe. Na wanawe wawili wakaoa wasichana wa Moabu. Lakini kama Mungu ameamuru kitu fulani kifanyike, kitafanyika hata hivyo. Hiyo ndiyo sababu ninaamini kabisa katika kuchaguliwa tangu zamani, kujua mambo tangu zamani kwa Mungu.

Ndipo tunaona, kule, mauti iliikumba familia, nao wakaanza kurudi. Ua ... Mvulana huyo alikufa, wavulana wote wawili walikufa, na baba naye akafa. Naye Ruthu akaanza kurudi, Orpa, na Naomi.

30 Sasa, ninataka kufananisha, asubuhi ya leo, Naomi, mama mkubwa, na kanisa la Othodoksi, kanisa la Othodoksi la Kiyahudi. Ruthu, Mmoabu, Mmataifa, akiwa ni Kanisa la Kikristo, Kanisa Jipya.

Nami nataka kuliendea, kutoka katika awamu nne mbalimbali, Ruthu. Nimeziandika hapa. Ruthu, akiamua, akifanya uamuzi wake; Ruthu, akitumika; Ruthu, akipumzika; Ruthu, akizawadiwa. Tunaporudi: Ruthu, akifanya uamuzi; Ruthu, baada ya kufanya uamuzi wake, basi Ruthu anahudumu; ndipo Ruthu anapumzika; ndipo Ruthu anazawadiwa.

31 Sasa, akiwa njiani akirudi, ulifika wakati, yeye akiwa ni mfano wa Kanisa, au Mkristo. Kwa kuwa, kila mtu anawakilisha taifa lote la Kikristo. Je! Ulijua jambo hilo? Wewe, katika matendo yako, jinsi utendavyo na kile ufanyacho, unawakilisha Mwili mzima wa Kristo. Unasema, "Lakini mimi ni mshiriki wa kawaida tu." Hilo halijalishi. Unapochukua jina hilo la Mkristo, unamwakilisha Kristo na Kanisa Lake. Unapaswa kuishi namna hiyo. Mnapaswa kuishi kama waungwana, kama mama wa heshima. Kamwe usifanye mambo ya ulimwengu, kwa sababu macho yote ya Mbinguni na duniani yametupwa juu yako, kuwakilisha kitu hicho kimoja. Haidhuru wewe ni mdhaifu jinsi gani, jinsi ulivyo mdogo, shikilia kichwa chako vizuri, maana wewe ni Mkristo.

32 Sasa, Ruthu alikuwa ni kafiri, aliabudu sanamu, na vivyo hivyo Orpa. Nao walikuwa njiani, wakirudi na mama mkwe. Kwa sababu, alisikia, kwamba, kule Bethlehemu ya Yuda, kwamba Mungu alikuwa ameondoa lile pigo, na watu walikuwa na chakula. Alikuwa huko juu kama miaka kumi, kwa hivyo Edersheim anasema, "kama miaka kumi," mwanahistoria.

Na kurudi, mwenye huzuni (naye mumewe amekufa, watoto wake wamekufa), pamoja na wakwe zake wawili. Kisha akageuka, hapana shaka, na kuwatazama, akasema, "Kwa nini mwende na mimi? Sasa, hamwezi kufanya lolote ila kupata matatizo." Kasema, "Nasikitika kwamba mkono wa Mungu umenyoosha dhidi yangu."

33 Ni mara ngapi Israeli wamefikiria hivyo, bila kujua kwamba yote yalikuwa ni mpango wa Mungu! Jinsi ukuta wa kuombolezea ulivyo tu nje ya Yerusalemu, ungali uko! Yale mawe ya kale ya hekalu, waliyaokota na kutengeneza ukuta. Nayo yamesuguliwa, kabisa, kwa machozi na kilio, kwa mikono ya Wayahudi, wakilia na kumsihi Yehova, "Yehova!" Hawatambui ya kwamba saa yao imekaribia sasa. Kuta za kuombolezea, "Mawe haya wakati mmoja yalilifanyia maskani lile Sanduku la Agano. Mfalme Daudi aliangalia mawe haya. Ee Yehova, uko wapi?" Mnaona? Bila kujua kwamba hivi karibuni Mfalme wake atarudi, Mkombozi wake. Ilibidi watupwe nje, kwa kipindi kidogo.

34 Naomi alishangaa, "Mbona mkono wa BWANA umenitendea ukatili sana, enyi wakwe zangu? Mungu amenitupa nje. Mimi nimetupwa. Sijui nimewahi kufanya nini, bali mimi nimetupwa." Mnaona?

Mungu alikuwa akitekeleza mpango Wake. Kwa sababu, "Vitu vyote hufanya kazi pamoja kwa manufaa ya wale wampendao Mungu," haijalishi ni nini.

Alisema, "Rudi kwa mama yako, na kupata raha katika nyumba za mama zenu. Waume zenu wamekufa. Nanyi ni vijana, wanawake warembo. Rudini. Rudini kule mlikotoka. Huko mpate raha. Mungu awarehemu, kwa sababu mlikuwa wema kwa wafu. Na mumeishi vema tangu waume zenu walipokufa. Na mmekuwa wema kwangu, mwanamke mjane mzee asiye na mume, na mkanishikilia. Rudini, na Mungu awape raha katika nyumba yenu." Wakalia.

35 Akasema, "Kama ... Mimi ni mzee. Nisingeweza kuwa na watoto zaidi. Lakini kama ningepata mume na kupata mtoto, ingefaa nini? Kamwe msingemngojea mtoto huyo." Hiyo hasa ilikuwa sheria katika siku hizo. Kwamba kama ndugu akifa, au...na, ninii yake, ndugu huyo mwingine akiwa hajaoa, ilimbidi amchukue mkewe ili kumwinulia jina kaka yake aliyekufa. "Lakini, yeye," kasema, "msingemngojea, watoto hawa. Kwa hivyo, rudini mkajipatie raha katika nyumba za waume zenu. Rudi kwa mama yako."

Basi, Orpa, mfano wa kanisa vuguvugu ambalo liliwahi kuanza, mfano wa kanisa ambalo halitaenda safari yote. Akasema, "Hilo linasikika zuri sana." Kwa hiyo, akambusu mama mkwe wake na kurudi tena. Huo ni mfano wa mwaminio vuguvugu, ambaye atamwamini Yesu kuwa ni Kristo, kisha ageuke na kurudi kwenye kitu ambacho ametoka. Kwa mtu ambaye atashika njia na wachache wa Bwana waliodharauliwa, halafu ageuke, arudi nyuma. "Kama mbwa kwa matapiko yake, na nguruwe kwenye kugaagaa kwake," kama Biblia ilivyosema.

36 Sasa, yeye alirudi kwa miungu yake. Mara nyingi tunarudi kwa miungu yetu ya—ya mwanzoni. Labda tuna macho ya kutamani kitu kibaya. Tutarejea kwenye tamaa mbaya tena. Labda tuna sanamu za

kunywa pombe, sanamu za kuvuta sigara, sanamu za uongo, sanamu za kuiba, kila namna ya sanamu; na halafu unakiri na kubatizwa, halafu unageuka tena. Ni jambo la kuhuzunisha iliyoje! Kumbukeni, halikutaja jina lake tena. Alitengwa kwa sababu ya uamuzi wake.

Kanisa vuguvugu, mwaminio vuguvugu, kwa kuwa kila mwaminio anawakilisha kanisa. Kila Mmarekani anaiwakilisha Marekani. Kila Mjerumani anaiwakilisha Ujerumani. Kila Mkristo anamwakilisha Kristo.

37 Huyu hapa aligeuza mgongo wake, kurudi kwenye kitu alichotoka. Jinsi ambavyo wanaume, hata wahubiri, wakati mwingine, watachukua njia ya Bwana, na unapozungumza nao juu ya ubatizo wa Roho Mtakatifu: "Upuuzi," wanamwondokea Huyo. Huyo ni Orpa.

Waambie kuhusu Jina la Yesu Kristo, kwamba, "Hakuna Jina jingine chini ya Mbingu walilopewa wanadamu liwapasalo kuokolewa kwalo. Lolote ufanyalo kwa neno na tendo, fanya yote kwa Jina la Yesu Kristo, ikiwa hakuna Jina jingine chini ya Mbingu likupasalo kuokolewa kwalo." Ndipo Petro akasema, kwenye ile siku, Siku ya Pentekoste, "Ukitaka kuokolewa, tubu na ubatizwe, katika Jina la Yesu Kristo, upate ondoleo la dhambi zako." Hivyo ndivyo zinavyoondolewa. Naye mtu, kwa sababu ya kupendwa na watu wengi, hawezi kushikilia Biblia juu yake. Lakini kwa sababu ya kupendwa na watu wengi, atalibusu Kanisa, atabusu Ujumbe, atabusu Kristo, "kwaheri," na kurudi kule alikokuwa ametolewa. Orpa, vuguvugu, aliyetengwa.

38 Lakini, loo, jinsi ninavyompenda huyo maskini Ruth! Ilimbidi kufanya uamuzi. Ilinibidi kufanya uamuzi. Huna budi kufanya uamuzi. Kamwe hutatoka nje ya milango hii, asubuhi ya leo, bila uamuzi wa namna fulani. Hutaondoka kwenye chumba hiki, leo, aidha ukiwa mwanamume ama mwanamke bora, ama mwanamume au mwanamke aliye mbaya zaidi. Kulikataa, utakuwa mbaya zaidi. Itakuwa vigumu zaidi wakati mwingine, kwako kulifikia. Ama, utatoka ukiwa bora zaidi.

Lilikuja shindano la kuamua maishani mwake. Linakuja shindano la kuamua katika maisha ya kila mtu. Na ilimbidi Ruthu kufanya uamuzi. Kwa hiyo, Biblia ilisema kwamba mama mkwe wake alimwambia, "Rudi kwa miungu wako kama vile dada yako alivyofanya. Rudi nyuma kama vile huyo mwenye uvuguvugu alivyofanya. Mbona usirudi nyuma."

Mhubiri wa Injili, "Ikiwa unataka kwenda, nenda." Mhubiri halisi na wa kweli atakayeliweka mbele ya darasa la watu, "Ninyi jiamulieni. Simameni kwa miguu yenu." Mwenye uvuguvugu, asiye na msimamo, mnyonge, hatasema hivyo. Lakini mtumishi halisi wa Mungu ataliweka mkononi mwako,

39 Ruthu akasema, "Nitaenda uendako. Watu wako watakuwa watu wangu. Mungu wako atakuwa Mungu wangu. Uishipo, nitaishi. Mahali utakapofia, nitakufa. Na mahali utakapozikwa, nitazikwa." Huo hapo uamuzi halisi.

"Bwana, nitakuchukua Wewe kama Mwokozi wangu. Kama Biblia ikisema, 'Tubuni mkabatizwe, katika Jina la Yesu Kristo,' hilo nitalifanya. Ikiwa Biblia ilisema 'lazima nipokee Roho Mtakatifu,' hilo nitafanya. Kama Biblia ikiniambia, 'Yesu Kristo ni yeye yule jana, leo, na hata milele,' hilo nitaamini. Nitachukua Biblia na Mungu, kwa yale aliyoadika na kile Yeye alicho, haidhuru mtu mwingine yeyote alisema nini." Huyo hapo Ruthu halisi.

Yeye alifanya uamuzi wake. Ilimbidi aidha kurudi nyuma ama kwenda mbele. Tunasimama kwenye uwanja ule ule, asubuhi ya leo, tunarudi ama tunasonga mbele. Usirudi nyuma kamwe. Hebu na tusonge mbele.

40 Moja kwa moja wakaingia katika nchi ya ahadi, katika nchi ya watu wageni. Ruthu, mfano wa mwaminio sasa. Kitu gani? Mwaminio ni nini? Wakati mwanamke ama mwanamume anapotoka, huyo mtu kutoka ulimwenguni, huingia miongoni mwa waaminio Wakristo. Wanawake waliozoea kuvuta sigara, kunywa pombe, na kucheza karata kwenye vyama, na kadhalika, na kuwa na kila aina ya vitu vya kupendeza, na kama aina fulani ya "ndege anayechachatika," lakini sasa amebadilika. Yeye amefanya uamuzi wa kwenda na Mungu. Sasa anaingia katika watu ambao hawaamini upuuzi wa namna hiyo. Yeye ni mgeni. Yeye hana budi kutembea kama msafiri. Yeye hajui desturi zao. Zote ni ngeni, kwake. Hajui la kufanya. Hivyo ndivyo ilivyombidi Ruthu kufanya. Hivyo ndivyo inavyokupasa kufanya. Hivyo ndivyo inanibidi kufanya.

Nilipomkubali Kristo, nilifukuzwa nyumbani kwangu mwenyewe. Nilipomkubali Kristo, marafiki wangu wavulana, marafiki wa kike, kila mtu, walinitupa chini. Nikashuka na kundi la wazee waliokuwa na Roho Mtakatifu na kumwamini Mungu, nikimtumikia yeye. Wasichana, waliokuwa huko chini katika kanisa hilo, walikuwa tofauti na wasichana ambao nilikuwa nikiambatana nao. Walionekana tofauti. Walitenda tofauti. Walikuwa wakipekee, nami niliwaogopa. Walikuwa watu tofauti.

41 Hivyo ndivyo ilimbidi Ruthu kufanya. Alilazimika kutoka kwa watu wake mwenyewe, kwenda kwa watu wengine. Alikuwa ameongoka. Alifanya uamuzi.

Nawe fanya uamuzi. Huna budi kufanya chaguo lako. Unataka kurudi kwenye mambo ya ulimwengu,



ama unataka kuendelea na Mungu?

Je! Unataka kutenda kama ulimwengu na hao wengine? Basi umbusu Kristo “kwaheri” na urudi nyuma.

Lakini kama unataka kuchukua njia yako pamoja na wachache wa Bwana waliodharauliwa, shikilia mkono wa Mungu usiobadilika. Haidhuru ulimwengu mwingine unasema nini, wewe shikilia papo hapo. “Mungu alisema hivyo. Ni kweli. Ninaamini jambo Hilo, ingawa siwezi kulidhihirisha maishani mwangu. Mungu alisema hivyo. Ninaamini jambo Hilo. Ninashikilia papa hapa.”

Hivyo ndivyo alivyomfanyia Naomi. “Sitakuacha. Nitaenda uendako. Watu wako watakuwa wangu. Jinsi wanavyotenda, hivyo ndivyo nitakavyotenda. Jinsi wanavyofanya, hivyo ndivyo nitakavyofanya. Kile wanachokula, hicho ndicho nitakachokula. Mahali utakapofia, nitakufa. Pale utakapozikwa, nitazikwa. Na Bwana anitendee zaidi ikiwa nitashindwa popote.” Huo ni uamuzi dhahiri kabisa. Mungu anataka maamuzi dhahiri kutoka kwa Kanisa Lake.

42 “Vema, Bwana, kama utanibariki tu na kunifanyia jambo *hili*, nitafanya *hivi na vile*.” Huo si uamuzi.

“Mungu, sijali utafanya nini nami, nitaenda hata hivyo. Kama nikifa, vema. Ishi au ufe, chochote kile! Kama wakinicheka, wakinidhihaki, halleti tofauti yoyote, nitaenda hata hivyo.” Huo ni uamuzi wa kweli, kama vile Rebeka alivyofanya kabla hata hajamwona Isaka.

Wazazi wake walisema, “Hebu msichana ajibu. Msichana huyo, yeye ni mtu mzima, acha ajibu.”

Akasema, “Nitaenda.” Uamuzi dhahiri kabisa, uliofanywa upesi. Aliushikilia. Hivyo ndivyo Ruthu alivyofanya. Orpa akarudi.

43 Wakasafiri. Ruthu, moyoni mwake, bila kujua anakokwenda, bali ni mfano wa Kanisa. Sisi ni wageni, kama Ibrahimu. Wasafiri katika nchi ya kigeni, miongoni mwa watu wa kigeni.

Ndipo akaendelea, na hatimaye akaingia chumbani na mahali ambapo Naomi alikuwa akimleta. Naye alipata nini? Kila mtu akimpigapiga mgongoni na kusema, “Ruthu, tuna furaha kuwa nawe hapa chini?” Alikuta ugomvi. Alikuta kitu kiovu. Alikuta matatizo.

Na wahubiri watakaokuambia kwamba, “Ma—maisha ya Kikristo ni raha mstarehe,” ama anakudanganya au hajawahi kupokea tukio hilo yeye mwenyewe. Ulimwengu unakuchukua. Nao watu watakuchukua. Huna budi kuchukua njia ya wachache wa Bwana waliodharauliwa, na kuchekwa, kudhihakiwa, ama cho chote kile. Huna budi kuwa tofauti. Umezaliwa na Taifa lingine.

44 Mke wangu ... Kama ni—nitakavyonukuu tena; inaonekana ni vizuri sana kunukuu. Akaniuliza, “Kwa nini wanawake Wakristo hawavai nguo hizo kama wanawake wengine wanavyovaa?” Nikasema ... Kasema, “Sisi sote ni Wamarekani, siyo?”

Nikasema, “La, bwana.”

“Vema, sisi ni nani?”

Nikasema, “Sisi siyo Wajerumani, Wafaransa, Wabelguimu, Waswisi, Waafrika, wala Wamarekani, siyo mmoja wao.”

“Lakini sisi ni nani?”

Nikasema, “Sisi ni Wakristo.” Wamarekani wanatenda kama Wamarekani, Wajerumani hutenda kama Wajerumani, kwa sababu hiyo ni roho yao ya kitaifa. Nasi tuna Roho wa taifa. Huyo ni Roho Mtakatifu akitoka kwa Mungu, kutoka Mbinguni, nawe unatenda namna hiyo. Inakufanya uenende kama wanavyofanya kule Juu, kwa sababu wewe ni wa Ulimwengu mwingine.

Tunaishi Marekani, hiyo ni kweli. Hiyo ni sehemu ya mwili. Bali nafsi inayotuongoza, tabia yetu, inatoka Juu. Tunaishi kutoka Juu kwa sababu tumezaliwa kutoka Juu. Wakristo wote wanatoka Juu. Yesu alisema, “Mimi si wa chini. Ninatoka Juu. Kama ningalikuwa kutoka chini, raia Wangu wangenipigania. Lakini Ufalme Wangu uko Juu.” Ndivyo ilivyo kwa kila mtu aliyezaliwa kwa Ufalme wa Mungu, yeye ametoka Juu.

45 Sasa, tukiangalia sasa. Tunapoendelea, tunawaona wakiudhika. Je, hapo ndipo ulipofikia, wakati ulipompata Roho Mtakatifu? Hakika nilipafikia. Nilipafikia. Kudhihakiwa, na kila kitu.

Halafu, angalia, maisha yalikuwa magumu kwake. Na ni vigumu baada ya wewe kuwa Mkristo. Kwa sababu unapaswa kujirekebisha kutoka kwa maisha ya aina moja, ya tafrija na raha za ulimwengu, kuingia kwenye maisha mengine, ya kujitolea kwa Mungu. Huna budi kujirekebisha, upande huu.

46 Basi ilimlazimu Ruthu kujirekebisha kutoka kuwa kwenye nchi ya chakula tele, na kila kitu kuheshimiwa, kuingia kwa watu waliokuwa wakimcheka, wakimdhahiki, hadi kwenye nchi aliyokusanya

masazo shambani apate chakula. Akayaweka kwenye skafu yake na kuyapeleka nyumbani. Na kuyapepeteta na kuoka mkate, naye na mama mkwe wake wakaula.

Alipokuwa huko, walikuja kujua, wakati alipokuwa akiokota masazo, au akienda kuokota masazo... Sasa, yeye alifanya uamuzi wake. Huo ulikuwa uamuzi wake.

Sasa, jambo la pili analopaswa kufanya ni kutumika.

Na hivyo ndivyo Kanisa linavyopaswa kufanya. Kanisa, baada ya kufanya uamuzi wenu, hamna budi kutumika. Mtumikieni Mungu kulingana na mpango Wake, kulingana na ramani Yake. Huna budi kumtumikia Mungu.

47 Ruthu, akifanya uamuzi. Sasa, Ruthu, akihudumu chini ya uamuzi wake. Sasa angalia kwa dakika moja tu. Sasa yeye anaenda kondeni, kuokota masazo.

Sasa, mama yake alimwambia; ambapo, Agano la Kale likiliambia lile Jipya, mnajua. Mama yake alimwambia, kasema, "Tuna jamaa, na jina lake ni Boazi. Yeye ni tajiri. Naye ni jamaa wa karibu. Nenda kwenye shamba lake. Na labda ... Usiende kwenye shamba jingine; nenda kwenye shamba lake."

Jinsi Roho Mtakatifu anavyotumia tusiende kando kwenye aina fulani ya ki—kitabu cha kanisa, aina fulani ya katekismo, lakini twende Shambani mwa Mungu, Agano la Kale, Biblia. Usiseme, "Vema, tutasema *hivi*. Nasi tutasema *hivi* kwa ajili ya maombi. Tutakuwa na *hili*." Kaa mumo humo Shambani. Nenda moja kwa moja ndani Yake, maana Yeye ndiye aliye Jamaa wa Karibu.

48 Neno la Mungu, Agano la Kale, ni Jamaa wa Karibu wa lile Jipya. Kanisa la Kale ni mama wa Kanisa Jipya, mnaona, Mkristo, mwaminio. "Usiende kwenye shamba lingine. Kaa mumo humo katika shamba lake. Na labda, siku moja, huenda ukapata neema kwake."

Na siku moja, alipokuwa huko kondeni, huyu kijana tajiri, jina lake Boazi, mtawala, mtu tajiri, alipita, naye akamwona. Loo, alipomwona, alimpenda. Alidhani alikuwa ni mwanamke mzuri sana. Alipenda tabia yake. Mnakumbuka, alisema, "Najua, halafu watu wanajua, ya kuwa wewe ni mwanamke mwadilifu." Alifanya uamuzi wake, safi na dhahiri. Akarudi moja kwa moja kule, akaishi vile vile hasa alivyosema angefanya.

49 Vinginevyo, leo, wao wanasema, "Tunajua ya kwamba wewe ni Mkristo. Tunajua ya kwamba wewe ni mtu wa Mungu, maana hakuna mtu awezaye kufanya miujiza hii isipokuwa Mungu awe pamoja naye."

Hivyo ndivyo Nikodemo alivyomwambia Yesu, alisema, "Rabi, tunajua ya kwamba wewe u mwalimu aliyetoka kwa Mungu. Hakuna mtu awezaye kufanya mambo unayofanya isipokuwa Mungu awe pamoja naye." Wakati, angeweza kumwona ameketi pale na kutambua mawazo ya moyo wao hasa.

Mwanamke aligusa vazi Lake. Akageuka, akasema, "Ni nani aliyenigusa?" Wote walikana. Akaangalia tena katika kusanyiko na kusema, "Wewe, unayetokwa na damu hapo, imani yako imekuponya."

Kasema, "Hakuna mtu anayeweza kufanya jambo hilo isipokuwa Mungu awe pamoja naye. Tunajua Wewe ulitoka kwa Mungu. Hatuwezi kukukubali, kwa sababu tutafukuzwa kanisani." Mnaona?

Huo mzabibu uliopandikizwa, Ndugu West, kama tulivyokuwa tukizungumza jana usiku, watakufukuza. "Lakini, chini moyoni mwetu, tunajua unatoka kwenye Mzabibu wa asili." Kristo ndiye Mzabibu; sisi ni matawi. "Tunajua, kwa sababu tunaona Uhai ule ule ulio ndani ya Mungu, umo ndani Yako."

Huo ndio Boazi alikuwa ameona kwa Ruthu, uamuzi huo dhahiri, uadilifu huo wa mwanamke aliyesimama pale. Naye akampenda.

50 Sasa, ninawatakeni mwone. Naomi, kanisa la kale, alianza kumwelezea Ruthu sheria zote kuhusu dini yake, kama vile Agano la Kale ni kivuli cha Jipya. Sasa, ninawatakeni mpate hadithi hii papa hapa.

Sasa, nataka kuonyesha vivuli. Agano la Kale linalielezea lile Jipya, kama tu utalisoma, kwa kuwa ni kivuli cha lile Jipya. Sasa, kama nilikuwa nikielekea kwenye ule ukuta, na sikuwa nimejiona mwenyewe, na nikione kivuli changu, ningejua, ningekuwa na dhana ya sura yangu. Na ikiwa (wewe) hujui Agano Jipya ni nini, soma la Kale nawe utaona kivuli chake. Mnaona? Na ndipo Agano Jipya linapoingia, unasema, "Mbona, hakika, hili ndilo." Kitabu cha Waebrania, tukirudi nyuma, Paulo akikielezea.

51 Sasa, angalieni kwa makini sasa. Wakati Ruthu aliposema, ama ... Naomi alipomwambia Ruthu, alisema, "Sasa, yeye ni jamaa yetu. Na kama unaweza kupata neema kwake, utapata raha." Loo, jamani! "Kama unaweza kupata neema, utapata raha." Boazi alimwakilisha Kristo, yule Tajiri, mrithi wa vitu vyote, Bwana wa mavuno. Loo, jamani! Jinsi ambavyo, wakati Boazi alipokuja amepanda farasi huko nje, katika lile gari, akiangalia kote mashambani, na macho yake yakamwangalia Ruthu! Alikuwa ni bwana. Yeye alikuwa bwana wa mavuno. Naye akapata neema machoni pake.

Hivyo ndivyo Kanisa linavyofanya, leo. Wakati Bwana wa mavuno akipita, Yeye haangalii jengo

kubwa, minara mikubwa, kwaya zilizofunzwa vizuri. Anatafuta watu binafsi, wanaume na wanawake ambao wamejitolea na kufanya uamuzi dhahiri kwa Kristo, waliojiweka wakfu kwa utumishi Wake. "Mungu, ninaamini Hilo, kila Neno Lake. Wakati Neno Lako linaposema jambo lo lote, ninakaa moja kwa moja Nalo. Hilo ni Neno Lako. Ninaamini Hilo, kila Neno." Hicho ndicho anachotafuta; Bwana wa mavuno. Hicho ndicho anachotaka kuwapa, Roho Mtakatifu, wale walio na njaa na kiu. "Heri ninyi wenye njaa na kiu, kwa maana mtashibishwa." Yeye anajaribu kulipata Kanisa hilo, leo.

52 Sasa, basi, Ruthu aliombwa kufanya jambo ambalo lilikuwa la aibu, bali alikuwa tayari kwa sababu alikuwa ameamua. Ni mfano wa jinsi gani wa mwaminio! Ni mfano mkamilifu ulioje!

Naomi, kanisa la kale, alisema, "Shuka uende, usiku wa leo. Ni msimu wa shayiri." Loo, ni wazo zuri iliyoje tungeweza kutegemea hapo!

Naomi na Ruthu walikuja tu wakati wa shayiri. Msimu wa shayiri ulikuwa ni msimu wa mikate, ule wakati ambapo mkate mpya ulikuwa ukitolewa. Nalo Kanisa, katika siku hizi za mwisho, kupitia miaka elfu mbili ya mafundisho ya kipagani na kadhalika, limeingia katika msimu wa shayiri, na Maisha mapya, Mkate mpya, asali kutoka Mbinguni. (Russell, zungumza juu ya mkate wa ganda la asali!) Huu Ndio, Mkate kutoka Mbinguni. "Mimi Ndimi Mkate wa Uzima. Baba zenu walikula mana, nao wamekufa. Lakini Mimi Ndimi Mkate wa Uzima utokao kwa Mungu, kutoka Mbinguni. Mtu akila Mkate huu hatakuwa kamwe." Nalo Kanisa katika siku hizi za mwisho hapa, linaletwa, sasa hivi, kwenye msimu wa shayiri.

53 Ruthu, Mmataifa, aliyetengwa, akafukuzwa, ameingizwa ndani, ili akubaliwe kama Bibi-arusi. Kristo aliingia, kwenye msimu wa shayiri tu.

Alisema, "Sasa jivike mavazi yako." (Siyo, "Vua mavazi yako.") Ni kinyume jinsi gani leo! "Jifunge mavazi yako, utakapokwenda kumlaki. Anaenda kupepeti shayiri, usiku wa leo. Shuka ujivike mavazi yako. Jifunike, ili kumlaki."

Siku hizi, wanataka kujifunua. Jifunikeni. "Shuka, kwa sababu anapepeti shayiri. Na kisha uangalie mahali anapolala." Ulifanya hivyo? Juu ya Golgotha. Miaka mingi iliyopita, niliweka moyoni mwangu mahali ambapo Yeye aliutoa uhai Wake, apate kunichukua. Paangalie mahali anapolala. Paangalie mahali alipolala. Hivyo ndivyo kila mwamini anavyopaswa kufanya. Angalia yale aliyokufanyia. Ujumbe wa Jumapili iliyopita, juu ya *Ziara ya Kalvari*, angalia yale aliyokufanyia.

54 Akasema, "Angalia mahali anapolala. Ndipo atakapojilaza chini kulala usingizi, kupumzika, nenda ujilaze miguuni pake." Sio kichwani mwake; miguuni pake, kutostahili. "Kisha uchukue blanketi" [Ndugu Branham anaipigapiga Biblia yake—Mh.] "aliyokuwa amejifunika nayo, ukajifunike nayo." Loo! Mnaona jambo hilo? [Kusanyiko linasema, "Amina."] Loo, jamani! Ninajua huenda mkadhani mimi ni mshupavu wa dini. Lakini huyo ananifaa tu vizuri, huyo Roho wa Mungu. Angalia mahali alipolala, Kalvari; mahali alipolala kaburini; huko Gethsemane. Tia alama, na utambae mpaka miguuni Pake. Lala pale na ufe, wewe mwenyewe, kwa ninii yako ... Haya basi. Jifunike, kabisa, na sketi Yake. Alisema, "Sketi," ndivyo alivyoita.

Naye Ruthu akasema, "Usemayo, nitayafanya."

Loo, ni uamuzi dhahiri iliyoje kwa mwaminio! "Yale Biblia isemayo, hayo nitafanya. Anasema, 'Tubuni mkabatizwe, Jina la Yesu Kristo,' nitafanya hivyo. Kama ikisema, 'Enendeni ulimwenguni mwote mkaihubiri Injili,' nitafanya hivyo. Kama ikisema, cho chote ilichosema, 'Yesu Kristo yeye yule jana, hata milele.' Kile inachosema nifanye, nitakifanya." Mnaona, Kanisa likichukua maagizo Yake kutoka kwenye Neno. Likajilaza chini.

55 Sasa, kumbukeni, hiyo ilikuwa ni fedheha kwa yule mjane mwanamke kulala karibu na mwanamume huyu, miguuni pake. Aibu, kwa ulimwengu wa nje.

Loo, unaweza kustahimili jambo hilo? [Kusanyiko linasema, "Amina." — Mh.] Hili hapa. Angalia. Angalia. Jambo ndilo hili. Kanisa, yule mwanamke kijana, mwanamume kijana, mzee au kijana, wanaombwa kujitenga na ulimwengu, na kuingia mahali, Ufalme wa Roho Mtakatifu, ambao ni aibu kwa ulimwengu. Moyoni mwao wanajua yote yanahusu nini. Lakini, kwa ulimwengu, wao wanakuwa washupavu wa dini. Wao wanakuwa mtakatifu anayejiviringisha ama kitu fulani juu ya wazo hilo, jina fulani la aibu. Lakini Kanisa linaombwa kufanya hivyo. Je! Uko tayari kuangalia mahali hapo, na kujilaza chini? ["Amina."] Acha ulimwengu ukuite chochote wanachotaka.

Ule wimbo wa kale, tuliozoea kuimba.

Nimeanza kutembea na Yesu peke yake, mnaona,  
Mto wangu, kama Yakobo, ni jiwe;  
Nami nitachukua njia na wachache wa Bwana waliodharauliwa;  
Nimeanza na Yesu. Ninapita.

56 Jambo ndilo hilo. Nitalipa gharama, hata wengine wafanye nini. Ikimaanisha fedheha, ikiwa

inamaanisha kupoteza makazi, kupoteza—kupoteza familia, wenzako wote, marafiki wa kike, marafiki wa kiume, vyovyote inavyoamaanisha, nitaenda peke yangu. Nitashika njia. Kama jirani yangu anasema mimi ni “mtakatifu anayejiviringisha, mpentekoste, ama mshupavu wa dini,” sijali wanasema nini. Haileti tofauti hata moja kwangu. Nimeanza kuingia. Nimeweka uamuzi wangu wazi, na ninapita.

57 Sasa, huyo ndiye peke yake angeweza kumpa raha, kutoka kwenye mashamba ya uchovu ya kuokota masazo. Loo, ilikuwa ni tamu sana wakati, Boazi, wakati alipompata huko shambani. Siwezi kukosa hili. Boazi alimkuta huko nje shambani. Akasema, “Angalia.” Akasema, “U nani wewe?”

Kasema, “Jina langu ni Ruthu.”

“Loo, yule Mmoabu aliyekuja kukaa pamoja nasi.”

“Naam.”

“Nimesikia habari zako. Huendi kwenye mashamba mengine.” Aha! Ninapenda hilo. “Usianze kutangatanga kwenye misheni. Kaa papa hapa shambani mwangu. Kaa na walio wangu.” Alimpenda. “Kaa hapa. Kaa pamoja nami. Usiende kutangatanga mahali mahali. Kaa hapa.”

Kama unaamini Ujumbe, ushikilie Huo. Mnaona? Haidhuru itagharimu nini, kaa nao. Endelea moja kwa moja. “Ikiwa inamaanisha, achana na *hili*, *lile*, au lile *lingine*. Nami sina budi kuacha kunywa pombe, sina budi kuacha wizi wangu, kusema uongo. Nitadumu nao moja kwa moja.” Mnaona?

58 Ndipo ikasemwa tena, akasema, “Sasa, hawatakusumbua, kwa sababu nimewaagiza vijana wasikuguse.” Amina. Ninapenda jambo hilo, ulinzi wake. Ni nani aliyesema hayo? Bwana wa mavuno.

Kuwa mwangalifu. “Msiwaguse watiwa mafuta Wangu. Msiwadhuru manabii Wangu.” Hiyo ni kweli? [Kusanyiko linasema, “Amina.” — Mh.] “Kwa kuwa amini, nakwambia, yakufaa sana kufungiwa jiwe la kusagia shingoni mwako, na kutoswa baharini, kuliko kumkosesha aliye mdogo zaidi wa hawa, wadogo Wangu.” Hiyo ni kweli? [“Amina.”] “Usiwakoseshe hata kidogo.”

“Nimewaamuru wasikuguse.” Loo, angalieni ulimwengu huo! Ni mtesi. Saa yao imekaribia.

59 Ndipo akawaendea wale vijana, hao wengine. Alisema, “Sasa, anakusanya masazo kwa ajili ya uhai. Sasa, ninawatakeni ninyi wavunaji ... enyi malaika,” kwa maneno mengine. Hivyo ndivyo walivyo. Kasema, “Nawatakeni nyinyi malaika, ninyi wavunaji, mara kwa mara, mwangushe konzi moja, makusudi.” Loo! “Msiache iwe ya kuchosha sana kwake. Lakini kila mara kwa mara, acheni asikie Ujumbe mzuri. Jalia nguvu nzuri za Roho Mtakatifu zimfunike, mara kwa mara, kumfanya ajue ya kwamba mimi bado nipo. Fanya namna fulani ya uponyaji miongoni Mwake. Onyesha namna fulani ya ishara au ajabu, apate kujua kwamba Niko miongoni Mwake.” Hivyo tu.

Hivi hampendi kupata makonzi hayo? [Kusanyiko linasema, “Amina.” — Mh.] Natumai tutapata kiasi asubuhi ya leo, sivyo? [“Amina.”] Konzi ya shayiri mpya. Bwana afanye kitu alichokuwa akifanya. Kitu ambacho tunajua Yeye hufanya. Yeye ni Bwana wa Mavuno. Yeye Ndiye pekee anayeweza kuangusha hiyo konzi. “Ninawaamuru Malaika waende kwenye mkutano huo asubuhi ya leo. Ninawataka wafanye jambo fulani, fulani. Nimewaagiza, nao watafanya hivyo.” Loo, jamani.

60 Sasa, hapa, ilimbidi achukue sehemu ya aibu, kulala chini, kuitwa chochote alichotaka. Angeweza kuitwa kahaba, mwajua. Angeweza kuitwa mwanamke mwenye sifa mbaya, hata hivyo hakuitwa. Naye alikuwa akifuata kanuni hasa alizopewa. Kwa hivyo yeye akashuka na kujifunika, kwa kifuniko alichokuwa amejifunika. Yeye angeenda wapi? Kaburini. Yeye angeenda wapi? Mahali alipokuwa akipumzika.

Hapo ndipo nilipoipata.

Pale msalabani alipofia Mwokozi wangu,  
Huko chini kwa ajili ya kusafishwa na dhambi nililia,  
Huko moyoni mwangu Damu ilitumika.  
Kuna Chemchemi iliyojaa Damu  
Inayotoka kwenye mishipa ya Imanueli;  
Ambapo wenye dhambi, wakijitumbukiza chini ya hayo mafuriko,  
Hupoteza waa lao lote la dhambi.

61 Angalia mahali alipojilaza chini, nawe ujilaze chini hapo pamoja Naye. Je, uko tayari kwenda Kalvari, asubuhi ya leo, kama nilivyosema Jumapili iliyopita? Umepaangalia mahali hapo maishani mwako? Je! Umefika mwenyewe mahali ambapo Yesu alisulubiwa?

“Loo, tunathamini jambo hilo.” Lakini vipi kuhusu kusulubiwa kwako? Uko tayari kuchukua njia pamoja na jina la fedheha, kama mtakatifu anayejiviringisha, shupavu wa dini, au chochote, chochote itakachogharimu?

Je, umeangalia mahali hapo, upate kwenda huko na kulala pamoja Naye, useme, “Bwana, mimi hapa?”

Kisha nini? Vuta kifuniko kile kile kilichokuwa juu Yake, ujifunike.

62 Mwanamke mmoja wakati mmoja alimwambia Bwana wetu, "Bwana, wajalie wanangu wawili, kwamba mmoja ataketi mkono wa kuume, na wa kushoto, katika Ufalme."

Akasema, "Je! Mnaweza kukinywea kikombe ninyweacho mimi?" Hayo ni yale mateso makali.

"Naam."

"Na mnaweza kubatizwa na ubatizo ambao nimebatizwa nao?" Jilaze chini, vuta kifuniko kile kile juu yake.

Eliya alitwaliwa juu. Naye Eliya akatupa chini kifuniko kile kile alichokuwa nacho, kumfunika Elisha kwa sehemu maradufu ya Roho wake. Jambo lile lile, sehemu maradufu tu. Nguvu zile zile; si zaidi. Si zaidi, si kubwa zaidi; sehemu maradufu tu Yake.

63 Kama vile Musa, wakati alipokuwa amechoka, baba mkwe wake alimwambia, kasema, "Unajichosha. Omba Mungu aichukue Roho yako na kuiweka juu ya wengine." Naye akaomba.

Ndipo Yeye akaichukua hiyo Roho na kuiweka juu ya wengine sabini nao sabini wakaanza kutabiri. Hawakuwa na nguvu zaidi. Walikuwa na mitambo zaidi. Hivyo tu. Kitu kile kile, walikuwa tu na mitambo zaidi.

Hivyo ndivyo ilivyo, leo. Mtu mmoja hawezi kufanya jambo hilo. Mungu ana mitambo Yake ikifanya kazi kila mahali, bali ni nguvu zile zile; nguvu zile zile, Roho Mtakatifu yule yule, Yesu yeye yule.

64 Sasa, alichukua blanketi, Roho Mtakatifu, wakati alipokufa peke yake. Akaangalia mahali alipofia, ambapo alijilaza chini kupumzika. Kisha akajilaza chini, akachukua blanketi iliyokuwa juu yake na kuivuta juu yake. Ndipo yule mtu akaamka, akasema, "Nani yuko hapo?" Yeye alisema ... Akasema, "Mimi ni Ruthu, Mmoabi, mjakazi wako."

Naye akainuka. Yeye alisema, "Ninaona na ninajua ya kwamba wewe ni mwanamke mwema." Amina. Loo! Je! Hivi hilo halisababishi mitetemo midogo nafsiini mwako? [Kusanyiko linasema, "Amina." — Mh.] "Wewe ni mwanamke mwema."

65 Naye alijibu nini? "Lakini wewe ni jamaa wa karibu." Amina. "Wewe ni jamaa wa karibu. Unaweza kunifanyia. Unaweza kunipumzisha. Nimekuja hapa na kujilaza hapa, sio kuwa mwanamke mtovu wa uadilifu. Nimejilaza hapa, sio kwa kujionesha; kuwaonesha watu ninaweza kunena kwa lugha, kuonesha watu ninaweza kucheza katika Roho, na kuwaonesha watu ninaweza kupaza sauti. Lakini nimekuja hapa kwa sababu wewe ni jamaa wa karibu. Sio kuonesha kuwa naweza kufanya kitu kikubwa; lakini wewe ni jamaa yangu. Nimekuja kwa sababu wewe ni jamaa wa karibu, na wewe ndiye pekee unayeweza kunikomboa."

Mnaona mtazamo wa—wa mwongofu kwa Kristo, kwa Kanisa? Mnaona? Mnaona? "Wewe ni jamaa yangu wa karibu."

Naye akasema, "Wewe ni mwanamke mwema. Nami ni jamaa yako wa karibu. Sasa, jifunike. Lala mpaka asubuhi." Whiu! "Jifunike tu kwenye blanketi hilo. Mimi ni jamaa yako. Lala hapo hata asubuhi, ukipumzika." Amina. Amina. "Mimi ni jamaa yako wa karibu. Pumzika!" Amina.

66 Kulipokucha, mapema kabla ya mapambazuko ya siku, alikusanya lundo kubwa la shayiri, vipimo sita, naamini ndivyo, na kuiweka kwenye maskini shela ya—yake akaenda nyumbani.

Na—na Naomi akasema, "Binti yangu."

Baada ya kuinuka kutoka madhabahuni, na kurudi. "Sasa itakuwaje, mama? Ni kitu gani kitakachotukia sasa?" Amina.

"Tulia." Amina. "Tulia, Ruthu, kwa sababu mtu huyo hatatulia hata atakapolipa gharama kamili ya ukombozi." Amina. Amina. Papo hapo ndipo ninaposimama. Amina. Yeye hatapumzika mpaka ametimiza gharama yote ya ukombozi, kukukomboa, kila kitu ulichowahi kupoteza, kila kitu ulichokuwa.

67 Sasa kumbukeni sheria ya ukombozi, tunapokaribia kumaliza, mwisho wa ibada. Sheria yote ya ukombozi ni hii, ya kwamba, kabla ya mtu kuweza kuikomboa mali iliyopotea, ilibidi awe wa jamaa aliye karibu zaidi. Na jambo la pili, ilimbidi awe mtu mnyofu, mtu mwenye haki, kufanya jambo hilo. Halafu ilibidi awe na mali ya kutosha, kufanya hivyo. Na ndipo ilimbidi kutoa ushuhuda wa hadharani ya kwamba alikuwa amefanya jambo hilo. Na tangu wakati huo na kuendelea, ilikuwa ni mali yake.

Kwa hiyo sasa angalieni. Boazi alimwakilisha Kristo. Sasa, Ruthu aliwakilisha Kanisa, wewe, mwaminio. Na sasa, Mungu, katika Agano la Kale, njia pekee ambayo Yeye angeweza kuja na kukomboa kile kilichokuwa kimepotea, ilibidi Mungu 'afanyike jamaa ya mwanadamu. Na njia pekee ambayo Mungu

angeweza kuwa jamaa ya mwanadamu, ilikuwa ni kuwa mmoja wao. Amina.

68 Ninatofautiana na Billy Graham, juu ya watu watatu mbalimbali katika Uungu, au mwalimu mwingine yeyote wa utatu, juu ya hilo. Ninaamini katika utatu, bila shaka, lakini si kwa namna hiyo, hao wakiwa ni watu watatu. Wao ni Mmoja. Hadithi hiyo pale, peke yake, haikuwa na kitu kingine ila hicho, ingelithibitisha.

Mungu alifanyika mwanadamu. Ilimbidi kuwa jamaa wa karibu. Mungu alifanyika mwanadamu. Ilibidi awe wa mbari. Wala asingeweza kuwa Mungu, na sisi wenye dhambi, viumbe vya uumbaji Wake, viumbe umbaji vya uumbaji Wake, maana hatungeweza kuwa wa jamaa moja huko. Kwa hiyo, Mungu alifanyika mwanadamu, ili mwanadamu apate kuwa Mungu, akawa Mungu. Amina.

69 Sisi, tukiwa watu, wenye dhambi, Mungu alifanyika mwenye dhambi, akajitwika dhambi zetu. Bila kujua dhambi, hata hivyo alikuwa mwenye dhambi kwa sababu dhambi zetu ziliwekwa juu Yake. Kwamba sisi ... Yeye alifanyika mimi, kusudi nipate kuwa Yeye. Mnaona? Yeye akawa mwenye dhambi, nipate kuwa mwana wa Mungu. Yeye alifanyika mwenye dhambi, upate kuwa mwana wa Mungu. Na sasa sisi ni wana na binti za Mungu, kwa sababu Mungu alifanyika jamaa wa karibu wakati alipochukua umbo la mwili wetu, alizaliwa na mwanamke. Mungu! Si mtu mwingine; Mungu, Mwenyewe.

Timotheo wa Kwanza 3:16 ilisema:

*... bila shaka siri ya utauwa ni kuu: Mungu alidhihirishwa katika mwili, ... Mungu!*

*Hapo mwanzo alikuwako Neno, huyo Neno alikuwa pamoja na Mungu, naye Neno alikuwa Mungu.*

*Naye Neno alifanyika mwili, ...*

70 Neno, lililofanyika mwanadamu, akawa wa jamaa. Yeye akawa mwanadamu. Loo! Alifanyika kifo, ili kwa kifo Chake niweze kuwa Uzima. Yeye alifanyika mwenye dhambi, ili kwa haki Yake nipate kuwa ... kupata Uzima. Akawa maskini, ili mimi, kwa umaskini Wake, niweze kuwa tajiri. Alifanyika kile nilichokuwa, ili kwamba mimi, kwa neema Yake, niwe kile alichu Yeye. Loo, jamani! Halafu, nena kuhusu nguvu za Mungu! Sasa, hayo ni Maandiko hasa. Na hivyo ndivyo Maandiko yasemavyo.

Ili kwamba tupate kuwa ... Je, ni upendo gani, ambao Baba amemwaga juu yetu, amemwaga juu yetu, kwamba sisi tuliokuwa wenye dhambi, wageni, mbali na Mungu, tupate kuvutwa karibu na Mungu, hata tunafanyika wana na binti za Mungu, sio watumishi. Kanisa la Mataifa kamwe si mtumishi. La, bwana. Kanisa la Mataifa ni mwana na binti. Ninyi ni wana na binti za Mungu, ambao mmempokea Roho Mtakatifu. Sasa, kama wewe ni kundi la Orpa, na ukageuka? Lakini mkiwa mmeendelea kupitia kwa Roho Mtakatifu, mnakuwa wana na binti.

71 Sasa, wana na binti, ni nani aliye na nguvu zaidi mbele za Mungu? Malaika ni nini? Malaika ni mtumishi. Hiyo ni kweli? Wao ni watumishi Wake. Wewe ni nini? Mwanawe na binti yake. Ni nani aliye na nguvu zaidi Mbinguni, basi, mwenye dhambi aliyeokolewa kwa neema, au Malaika Mkuu anayesimama upande Wake wa kuume? Mwenye dhambi, ambaye ameokolewa kwa neema, ana mamlaka zaidi Mbinguni kuliko yule Malaika Mkuu aliyesimama kando Yake, bila dhambi, maana yeye ni mwana. Mwana ana mamlaka zaidi kuliko mtumishi, bila shaka.

Loo, tunasahau tulivyo. Tunasahau, mara nyingi, kile kilichotufanya tulivyo. Baada ya sisi kuwa vile tulivyo, basi tulisahau jinsi tulivyofika hapa. "Wakati Mungu Mwenyewe ..."

Loo, ni upendo wa thamani iliyoje Baba  
Aliipa jamii ya Adamu iliyoanguka;  
Alimtoa Mwanawe wa pekee kuteseka  
Na kutukomboa kwa neema Yake.

Loo, jinsi tunavyopata kujua!

Huku miamba ikipasuka na anga zikiingia giza,  
Mwokozi wangu anainamisha kichwa Chake na kufa;  
Pazia lililofunguka liliifunua njia  
Ya kuenda kwenye furaha ya Mbinguni na siku isiyo na mwisho.  
Juu ya Kristo, Mwamba wenye imara, nasimama;  
Sehemu zingine zote ni mchanga udidimiao.  
Ninapochunguza msalaba wa ajabu  
Ambapo Mfalme wa Utukufu alikufia,  
Ninahesabu dhambi zangu zote kuwa hasara.

Hiyo ni kweli. Mmoja alisema:

Alipoishi, alinipenda; alipokufa, aliniokoa;  
Alipozikwa, aliziondolea mbali dhambi zangu;

Alipofufuka, alinihesabia haki bure milele:  
Siku moja Yeye anakuja. Loo, siku tukufu.

72 Limekuwa ndilo somo la Kanisa. Umekuwa ndiyo mtazamo Wake. Umekuwa ndiyo moyo Wake. Dunia hii imeoshwa na Damu ya huyu Mkombozi Aliye Jamaa Wa Karibu, kuikomboa jamii ya Adamu iliyoanguka.

Angalieni, huyu hapa, Mkombozi Aliye Jamaa wa Karibu. Sasa, jambo la kwanza, ilimbidi awe mtu anayestahili. Ni nani aliyestahili zaidi kuliko Kristo, kuliko Yesu? Halafu, jambo lingine, ilimbidi awe na pesa. Ilimbidi awe na uweze wa kufanya hivyo. Alimiliki Mbingu. Alithibitisha alizimiliki. Angeweza kuchukua mikate mitano na samaki wawili, na kuwalisha elfu tano, wakaokota vikapu vitano vilivyojaa vipande, baadaye. Angeweza kuvuta maji kwa pampu kutoka kwenye kisima na kuyabadilisha yakawa divai. Angeweza kumtoa samaki kutoka baharini, na kutoa sarafu kinywani mwake, za dhahabu. Amina. Yeye hakuwa ...

Lakini Yeye akawa maskini, hana mahali pa kulaza kichwa Chake. Yeye akawa Jamaa wa Karibu. Si Jamaa wa Karibu kwa matajiri; Jamaa wa Karibu kwa watu wote. Yeye alichukua mahali pa mkombozi.

73 Basi ilimbidi kufanya nini? Ndipo ilimbidi kutoa ushuhuda hadharani. Kesho yake asubuhi, Ruthu akasema ... Ama, Naomi alisema, "Tulia, Ruthu. Kila kitu kitakuwa sawa sasa, kwa sababu umepata neema mbele zake."

Mungu, hebu nifanye hivyo. Hebu nipate neema mbele Zake. Ndipo kutakapopambazuka:  
Baragumu Yake Bwana wakati ikipigwa, na hapatakuwapo na wakati tena,  
Na asubuhi ipambazuke, Milele, angavu na nzuri;  
Na wakati waliookolewa duniani watakapokusanyika kwenye ule ufuko mwingine,  
Majina yaitwapo huko ng'ambo, nitakuwapo.

74 Tunatulia sasa, tusingojea ukombozi mkamilifu. Angalia, ninayo, ile—ile arabuni Yake, sasa. "Nilipeleka nyumbani skafu nzima iliyojaa shayiri. Nilifika pale." Akampa, akaipima, vipimo sita. Sita, ilimaanisha, "ile miaka elfu sita ya kuwako kwa ulimwengu." Siku ya mwanadamu ni sita. Mwanadamu aliumbwa siku ya sita. Kutakuwako na miaka elfu sita ambapo ulimwengu uliumbwa, katika ile elfu ya saba Mungu alipumzika. Miaka elfu sita Kanisa litajitahidi dhidi ya dhambi, kwa Nguvu za Mungu za mikate hii ya shayiri, na kisha kuingia katika Raha ya Milele. Kweli. Raha, subiri. Akaweka vipimo sita vya shayiri safi, kumpeleka mpaka wakati wa ukombozi mkamilifu. Nina furaha sana kuufurahia.

75 Sasa, upesi, hebu tufikie mwisho wake. Sasa tunaona, sasa, ya kwamba, kesho yake asubuhi, alipoamka, alikuwa na furaha, akingojea. Ndipo yule mtu akaja. Akashuka. Alikuwa na jamaa mwingine ambaye kweli alikuwa na haki juu ya mwanamke huyo, kwanza. Je! Nina wakati wa kupata jambo hilo? [Kusanyiko linasema, "Amina." — Mh.] Vema, hebu kidogo, nasi tutapata sehemu yake, hata hivyo.

Yule wa pili katika huo mfano, ambaye alikuwa na nafasi juu yako, alikuwa ni ibilisi, maana ulikuwa umetenda dhambi. Na kwanza wewe ulikuwa ni wake, maana, ulikuwa, wewe ni mali yake. "Kwa maana ulizaliwa katika dhambi, ukaumbika katika uovu, ukaja ulimwenguni ukinena uongo." Naye hangeweza kuikomboa. Mnaona? Asingeweza kuikomboa. Kwa hiyo, Kristo alikuja na akafanyika mwanadamu, kuziondoa dhambi zetu, kutukomboa. Mnaliona hilo? [Kusanyiko linasema, "Amina." — Mh.] Na mtu huyo mwingine asingeweza kufanya hivyo. Ibilisi asingeweza kufa kwa ajili ya dhambi, kwa sababu alikuwa mpotoshaji hasa aliyefanya dhambi. Mnaona? Asingeweza. Angeharibu urithi wake, jamaa huyo mwingine. Naye Shetani angeuharibu yake, kwa sababu yeye ni ibilisi. Asingeweza kuwa ibilisi mwingine, kumwondoa Ibilisi, ibilisi wa kwanza. Asingeweza kuwa dhambi, maana tayari alikuwa dhambi. Lakini, Kristo, akiwa hana dhambi, alifanyika mwenye dhambi. Angeweza kutukomboa. Haleluya! Tumekombolewa. Sisi tumekombolewa, maana yake, "kurudishwa." Tumekombolewa.

76 Kwa hiyo, kesho yake asubuhi, ndipo ilimbidi kutoa ushuhuda wa hadharani. Akashuka akaenda na kukutana na mtu huyu langoni, mbele ya wazee. Na ilibidi iwe mahali pa hadhara. Naye akamwangalia usoni. Akasema, "Waweza kumkomboa?" Sasa, ilimbidi amkomboe Naomi kwanza, ili ampate Ruthu; Naye Kristo ilimbidi alikomboe kanisa la Kiyahudi, kwanza, kusudi ampate Bibi-arusi wa Mataifa. Yeye alikuja pamoja na Naomi, kama mgeni kutoka nchi nyingine, Mmoabu, wapagani. Hivyo ndivyo tulivyokuwa, Mataifa, mpagani. Na kumbukeni, ilimbidi—ilimbidi kumpata Naomi. Na wakati alipompata Naomi, alipata yote aliyokuwa nayo.

77 Kumbukeni, Kristo alipokuja, Yeye hakunena kamwe juu ya Kanisa la Mataifa. Ilikuwa ni, kwenda kwa walio Wake, "Yeye alikuja kwa walio Wake. Walio Wake hawakumpokea." Yeye daima alikuwa kwa walio Wake. "Msiende katika njia ya Mmataifa. Msiende Samaria, bali nendeni hasa kwa kondoo wa Israeli waliopotea. Na mnapoenda, hubirini Injili, waponyeni wagonjwa, wafufueni wafu, watoeni pepo. Mmepokea bure, toeni bure." Hiyo ni kweli? [Kusanyiko linasema, "Amina." — Mh.] Akawatuma, wawili wawili. Nenda kwanza ... Naye ilimbidi kulikomboa kanisa hilo. Na wakati alipolikomboa kanisa hilo, Yeye alipata Bibi-arusi Mmataifa. Amina. Hayo yalikuwa ndiyo makubaliano yake. Mnaona? Alimpata Bibi-arusi wakati alipolikomboa kanisa.

78 Sasa, Boazi, ilimbidi kutangaza hadharani ... Akasema, "Waweza kumkomboa?"

Akasema, "La."

Ndipo ilimbidi kutoa ushuhuda wa hadharani. Alivua kiatu chake, na kumtupia. Kasema, "Haya basi. Israeli wote na wajue kwamba nimemkomboa Naomi, na pia nimemchukua Ruthu." Amina. "Ninamchukua Ruthu kuwa bibi-arusi wangu." Alikuwa ni nani? Bwana wa mavuno. Amina. Huyu hapo. "Ninamkomboa Naomi, na ninampata Ruthu. Na Ruthu atakuwa bibi-arusi wangu."

Wangesema nini? "Na awe kama—kama Lea na Raheli na hao wengine, aongeze maelfu," naye amefanya hivyo, hiyo ni kweli, "kwa Israeli. Jalia awe hivyo." Na, angalia, alifanya jaribio, ushuhuda wa hadharani.

79 Yesu alifanya nini, kufanya jambo hilo? Yeye alitoa ushuhuda wa hadharani. Wakati, Shetani asingeweza kufa kwa ajili ya dhambi kwa sababu alikuwa mwenye dhambi. Yeye ni baba wa dhambi. Lakini, Yesu, Yeye asiye na hatia, Mungu wa Mbinguni, ambaye haikumlazimu kufa, alishuka akashuhudia hadharani kwa kufa, akainuliwa juu kati ya mbingu na nchi. Ushuhuda wa hadhara; akavuliwa nguo Zake, na kuning'inia kati ya mbingu na nchi, katika aibu. Na akafa, kifo cha dhambi, cha aibu, kutukomboa. Ushuhuda wa hadharani! Amina.

Yeye alifanya nini? Aliiondoa haki Yake mwenyewe; akautoa utukufu Wake mwenyewe. Akaondolea... "Ninazo nguvu. Ningenena na Baba Yangu, na mara moja angenitumia vikosi ishirini vya Malaika." Wangeweza kuubadilisha mwelekeo. Malaika mmoja angaliweza kufanya hivyo. Angeweza kuagiza vikosi ishirini. Hiyo ingekuwa ni kama Malaika elfu arobaini. Wangeweza kufanya nini? Yeye alisema, "Ningeweza kuzungumza na Baba Yangu, mara moja, hiyo ni sasa hivi, Yeye angenitumia vikosi ishirini. Jeshi la Malaika litakuja hapa na kutwaa hili." Mtu angefanya nini? Mtu angeiangamiza dunia, katika sekunde moja. Angalia tu, Yeye alikuwa na maelfu wangaliweza kuja. Mnaona? Lakini Yeye aliliondoa hilo. Aliweka hilo kando. Yeye aliweka heshima Yake yote, kila kitu, kando, na akawa mwenye dhambi na akafa kwa ajili yako na mimi.

80 Sasa, katika kufunga, huenda tukasema jambo hili, katika kufunga. Yeye alifanya—alifanya hivyo. Ndipo akamchukua Ruthu, naye akamwoa. Naye akamzaa mwana aliyeitwa Obedi. Obedi alikuwa baba wa Yese. Yese alikuwa baba wa Daudi, ambaye alikuwa baba wa Kristo, amina, baba wa Bwana Yesu.

Hivi hamwoni? Kupitia haki hiyo, kupitia huo uamuzi ulio dhahiri, Yeye alifanyika Mkombozi Aliye Jamaa yetu wa Karibu. Mungu alifanyika jamaa yetu, kushuka na kufanywa kama sisi, mwanadamu, kuona njaa, kupata kiu. "Ninaona kiu. Nipe maji ninywe." Nao wakatia siki kinywani Mwake, nyongo. Yeye aliona kiu kama tulivyoona. Alijua jinsi ya kuishi bila kitu.

Alikuwa mgonjwa kama sisi. Alisema, "Je, si wataniambia methali ya kale, 'Tabibu, jiponye nafsi yako?'" Lakini nguvu Zake kuu hazikuwa kwa ajili Yake Mwenyewe. Alikuwa na nguvu za kufanya hivyo, lakini asingeweza kuzitumia kwa nafsi Yake. La.

81 Mtu fulani aliniambia, hivi majuzi, alisema, "Ndugu Branham, kabla jambo lolote halijatukia, unajua yote yatakayokupata."

Nikasema, "Karama hiyo si kwa ajili yangu. Siwezi kuitumia kwa ajili yangu mwenyewe." Ni kwa ajili yenu. Ninyi ndio mnaopata faida, siyo mimi. Mimi ni mtumishi tu wa umma wa Mungu, kwenu.

Mhubiri ni mtumishi wa umma. Anajishikilia tu hapo. Kama vile yungiyungi la kondeni, nyukibambi hurukia, anapata sehemu yake. Nyuki wa asali huruka na kupata yake. Mpita njia anapata yake, na kila kitu. Yeye hutenda kazi, mchana na usiku, lipate kuendelea linawiri. Naye mhudumu wa Injili hufanya jambo lile lile; anatembea katika mstari wa Mungu. Anashikilia ushuhuda wake vema, ulimwengu upate kumshiriki, mnaona, Bw. Mchungaji Yungiyungi. Yeye ni mzuri. Yesu alisema, "Mtafakarini. Sulemani si kama yeye." Hiyo ni kweli. Dk. Yungiyungi, nadhani nyote mnamfahamu. Mnaona?

82 "Yatafakarini maua ya kondeni, jinsi yanavyotenda kazi na kusokota, wala. Nasema, na, hata hivyo, Sulemani, katika fahari yake yote..." Yungiyungi halina budi kujitahidi, mchana na usiku, lipate kunawiri lihifadhi mavazi yake, kuyaendeleza manukato na kadhalika. Na wengine ... Yeye hujifunua tu mwenyewe, na wanakuja na kuyatoa kwake. Nyuki na nzi, na kila kitu, huja hapo, wema au wabaya, huchukua tu kutoka kwake.

Hivyo ndivyo alivyo mtumishi, wa Kristo, mtumishi Mkristo; hujifungua mwenyewe, "Ondoa tu kutoka kwangu, ulimwengu." Hakuna kitu kwa ajili yake mwenyewe. Ni kwa ajili ya hao wengine. Hivyo ndivyo Kristo alivyokuwa wakati alipofanyika jamaa yetu. Yeye alifanyika mwanadamu, ili ulimwengu upate kushiriki haki Yake, mnaona, na kufanywa wana wa Mungu.

83 Sasa, walifanya nini? Walioana, na kupitia jambo hilo kukaja jambo hili kuu. Ndipo Ruthu alipewa thawabu, kwa kumpata Kristo ... ama kumpata Boazi kwa ajili ya mumewe. Ambapo, Kanisa limepewa



thawabu, hapo Kuja kwa Bwana kutakapotukia, katika asubuhi hiyo angavu na isiyo na mawingu. Tunapumzika, tuingojea sasa. Itakuja. Sasa, kwa nini? Imekombolewa.

84 Sasa, nukuu moja zaidi kabla sijaondoka, kuanzisha mstari wa maombi. Nukuu moja zaidi. Nilichunguza, asubuhi ya leo, neno *komboa*. Nilininii tu ... Samahani, enyi ndugu zangu wa Kiarmenia, bali inanibidi tu kuingiza hili ndani; si kuwaudhi, bali kuwafanya tu kuwazia. Chunguzeni kile *ukombozi* unachomaanisha. Ukombozi, kweli ulitumika, katika neno la Kiyunani, kumtoa mtumwa sokoni. Siwezi kutaja herufi za hilo neno la Kiyunani sasa, bali linamaanisha, "kumchukua mtumwa kutoka sokoni," *kukomboa*.

Mtu fulani amefanya jambo fulani baya, kwa hiyo, yeye, bwana wake alimwaza utumwani, haswa hata kifo. Naye yuko sokoni, yeye ni mtumwa. Lakini mtu anakuja, mtu anayestahili anayeweza kufanya jambo hilo, na kumpata mtu huyu, na kupata neema machoni pake, anamkomboa. Hilo linamwondoa kwenye soko la watumwa, na kumpeleka nje kwake mwenyewe. Angalia. Na huyo mtumwa, akikombolewa mara moja, hawezi kuuzwa sokoni tena. Amina. Hawezi kuuzwa tena. Ametiwa alama. Na kama alifikiriwa vya kutosha, wakati mmoja, kukombolewa, hakuna mtu anayeweza, kamwe, kumuuzwa tena kama mtumwa.

85 Loo, ashukuriwe Mungu, ya kwamba wakati mtu amemjia Kristo mara moja na amekombolewa kwa Damu ya thamani, Ibilisi hawezi kukufanya mtumwa tena. Uko salama katika Damu ya Yesu Kristo hata siku ya ukombozi wako. Mtumwa, liangalie katika Kutoka, uone kama hizo si sheria za Walawi. Ninamaanisha, katika Mambo ya Walawi, angalia kama hizo si sheria. Mtumwa, akikombolewa mara moja, hawezi kuuzwa tena kuwa mtumwa. Hiyo ni kweli.

Loo, nina furaha sana! Nina furaha sana kujua ya kwamba Mkombozi wetu aliye Jamaa wa Karibu, kwamba Mungu wa Mbinguni, Ambaye alikuwa Roho, alishuka duniani na akafanyika mwili; alifanywa kama nilivyo mimi, alifanywa kama ulivyo wewe; na kuchukua umbo la mwili wenye dhambi, bila kujua dhambi, ili dhambi zetu ziwe juu Yake; na kuwa jamaa yetu, alifanyika ushuhuda wa hadharani wa kufa, kulipa gharama kamili.

Na Roho wa Mungu akishuhudia tena. Hekalu lilipasuliwa, lile pazia, kutoka juu hata chini. Si kutoka chini hadi juu, bali kutoka juu hadi chini; ilionyesha ilikuwa ni Mungu, Mwenyewe, aliyelirarua, kutoka Juu. Akalirarua kutoka juu hadi chini, na kuifungua njia. Ndipo matofali ya dhabihu yakageuzwa, na radi ikamulika kwa miale yake gizani, anga zenye hasira. Jua likatua katikati ya mchana. Nyota zilikataa kung'aa. Na kila kitu kinatoa ushuhuda, "Tumekombolewa." Haleluya!

Hebu na tuombe. [Ndugu fulani anatoa tamshi la kinabii — Mh.]

86 Huku vichwa vyenu vimeinamishwa sasa, kwa muda kidogo tu. Hayo yalikuwa matamshi ya kinabii, kuliita kanisa, baada ya Ujumbe.

Sasa kama kuna baadhi hapa ambao hawamjui, maisha yenu si sawa, mmealikwa sasa kusimama hapa mbele ya wasikilizaji hawa, uso wa Mungu, kumkubali kama Mwokozi wenu. Maji yamo kwenye kidimbwi cha ubatizo. Kama mtu fulani akingojea kuanza ibada ya ubatizo, mara moja.

87 Huku tumeinamisha vichwa vyetu, tutachukua wakati huu sasa kwa kuimba *Ninapitia*. Huku vichwa vyenu vimeinamishwa sasa.

Ninapitia, naam, ninapitia,  
Nitalipia gharama, haidhuru wengine wanafanya nini;  
Nitashika njia pamoja na wachache wa Bwana waliodharauliwa;  
Nimeanza na Yesu, nami ninapitia.  
Ninapitia, naam, ninapitia. Mimi ...

Unamaanisha kweli sasa? Kama ndivyo, njoo hapa na usimame.  
... haidhuru wengine wananya nini;  
Nitachukua njia ...

Je, uko tayari kushikilia, kama Naomi wa kale?  
Nimeanza pamoja na Yesu, nami ninapitia.  
Kutoka hori ya Bethlehemu akaja Mgeni,  
Duniani ninatamani kuwa kama Yeye;  
Kote katika safari ya maisha kutoka duniani hadi Utukufuni,  
Ninaomba tu kuwa kama Yeye.  
Kuwa kama Yesu, ...

Unataka kuwa kama Mkombozi wako?  
... kama Yesu,  
Duniani ninatamani kuwa kama Yeye;  
Kote katika safari ya maisha kutoka duniani hadi Utukufuni,

Naomba tu kuwa kama Yeye.  
 Niangazie, Bwana, niangazie,  
 Nuru kutoka kwenye Nyumba ya taa iniangazie;  
 Niangazie, Bwana, niangazie,  
 Jalia Nuru kutoka kwenye Nyumba ya taa iniangazie.  
 Kuwa kama ...

Kulikuwa na mtu mwingine yeyote ambaye ungependa kuwa kama Yeye, zaidi ya Yeye? Hivi mtu mwingine hatakuja sasa na kupiga magoti hapa pamoja na msichana huyu, anapopiga magoti? Kushika, kama Ruthu wa kale, kushika njia yake asubuhi ya leo.

... kama Yeye;  
 Kote kote ... duniani hata Utukufuni,  
 Naomba tu kuwa kama Yeye.  
 Kuwa tu kama Ye- ...

Mtu mwingine aje sasa. Atembee hapa chini na kupiga magoti, kama mama huyu alivyofanya hapa. Umeanza? Utaweka mikono yako katika Yake?

Natamani kuwa kama Yeye;  
 Kote katika safari ya maisha kutoka duniani hadi Utukufuni,  
 Naomba tu kuwa kama Yeye.

[Ndugu Branham anaanza kuvumisha *Kuwa Kama Yeye* — Mh.]

88 Baba yetu wa Mbinguni, wakati kanisa likiuvumisha wimbo huu, "kuwa kama Yesu," mwanamke huyu, asubuhi ya leo, ametoka, kama Ruthu. Ina Bell, akija kama Ruthu wa kale. Haidhuru gharama yake ni nini, yeye amekuja kulipa. Haidhuru nini ... jinsi atakavyochekwa, ama kudhihakiwa, anachukua mahali hapo sasa, amesimama hapa, akikiri dhambi zake. Akipiga magoti, akiangalia mahali ambapo Bwana mkubwa wa mavuno alilala msalabani. Na pale kupokea Roho Wake, neema Yake iliyosema naye wakati Neno lilipokuwa likitoka, kama Naomi wa kale, akielekeza. Nayo ilimgusa anayefaa, mahali sahihi. Na sasa anakuja kuchukua mahali pa mwaminio, akipiga magoti msalabani, hapo ambapo anakiri dhambi zake, anaweka kando mambo yote ya kale ya maisha, na anakuwa kiumbe kipya katika Kristo Yesu.

89 Tunaomba, Baba, asubuhi ya leo, ya kwamba kila mtu aliyetengwa katika jengo hili, kila mwanamume, mwanamke, mvulana, ama msichana, asiyekujua Wewe, usiache Maneno haya yapite, Bwana. Hatujui ni saa gani tutakayoingia Hukumuni. Huenda inawezekana kwamba leo hii ndiyo wengi wetu ikatulazimu kuja. Labda kabla hatujafika nyumbani, ajali itatokea. Huenda ... Shambulio la moyo linaweza kutupata. Hatujui. Ee Mungu, hebu na tujiweke tayari, saa hii, wakati Roho yupo hapa, wakati tukiwa na ushuhuda ya kwamba Yeye yuko hapa, wakati Mungu wa Mbinguni, katika rehema Zake zote zisizo na kikomo, yuko hapa kutuingiza.

Tupe neema Yako, Bwana. Watume wengine, asubuhi ya leo, madhabahuni, na kumkubali Kristo kama Mwokozi, kama mwanamke huyu anavyofanya sasa. Tujalie, Bwana. Mhurumie, ukijua ya kwamba watu wake ... Ndugu yake ameketi hapa jukwaani pamoja nami. Dada yake, Wood, akiketi pale nje; mama na baba wamekaa hapa. Bwana Mungu, ninaomba rehema. Tujalie, Bwana. Mnajua ninalomaanisha moyoni mwangu. Ninaomba ya kwamba kumwaga Kwako kwa Damu Yako, katika rehema, kutakuja sasa kwenye saa hii. Tujalie, Bwana. Jalia, tunapowangojea wengine, jalia wengine waje, pia, Baba, na wapatanishwe na Mungu kwa njia ya Kristo.

90 Na sasa, wakati tunangojea sasa na kushangaa, tutaimba tena.

Niangazie, Ee Bwana, niangazie.  
 Jalia Nuru hiyo kutoka kwenye Mnara wa taa iniangazie.

Vema. Naam.  
 Niangazie ...

Je! Kungekuwa na mwingine anayekuja?

... Niangazie,  
 Jalia Nuru kutoka kwenye Mnara wa taa iniangazie;  
 Niangazie, Bwana, niangazie,  
 Jalia Nuru Yako kutoka kwenye Mnara wa taa, iniangazie ...

Itanifanyia nini?

Kuwa kama Yesu, kuwa kama Yesu,  
 Duniani ninatamani kuwa kama Yeye;  
 Kote katika safari ya maisha kutoka duniani hadi Utukufuni,  
 Naomba tu kuwa kama Yeye.

91 Baba Mungu, huo ndio ushuhuda wetu kweli. Bwana, tunataka kufanana na Yeye, wapole na

wanyenyekevu, waliojitweza, watamu, daima akiwasamehe wale wanaomtendea vibaya na kufanya vibaya. Tu—tunataka kuwa hivyo. Tunakushukuru kwa ajili ya mwanamke huyu aliyekuja asubuhi ya leo. Tunajuaje maisha haya yatakuwaje, baada ya kitambo kidogo? Labda kupitia makosa yake yote na kadhalika maishani, kama sisi sote tumefanya, tukiwaona wamezama chini ya mafuriko asubuhi ya leo. Ninaomba, Mungu, kwamba mwanamke huyu ataishi maisha yaliyowekwa wakfu yatakayowaongoza wenzake wote kwenye ujuzi huu. Jalia asikomee hapa, bali aende aingie katika nchi ya ahadi, akipaangalia mahali hapo na kujilaza chini, ampokee Roho Mtakatifu hapo. Tujalie, Bwana.

Kama kuna wengine zaidi humu ndani, Baba, ambao walipaswa kuja, wala hawakuja, Roho Wako asiwaache. Jalia wasipate raha, mchana wala usiku, mpaka wao wamekuja, pia, wamefanya uamuzi huu huu. Siyo kuwa mkali, Bwana, lakini, Ee Mungu, nikijua wanachokosa. Kujua itakavyokuwa kwenye Siku ile, kumsikia Yeye akisema, "Ondokeni Kwangu, ninyi mtendao maovu. Asubuhi hiyo, katika Mtaa wa Nane na Penn, nilikuita, wala hukuja." Ee Mungu, hilo lingekuwa ni saa ya kutisha jinsi gani kwao, tunapopimwa mizani na kuonekana tumepungukiwa. Baba, jalia ya kwamba hilo halitamjia mtu ye yote katika Uwepo wa Kiungu. Jalia wote waokolewe. Tunaomba katika Jina la Yesu. Amina.

92 Tunataka kumshukuru Bwana, asubuhi ya leo, kwa wema Wake na fadhili Zake. Ninawashukuru nyote kwa saburi yenu, ya kungojea pamoja nami kwa muda mrefu.

Dada Ina Bell. Mimi ... Dada Wood, huyo ni dada yako, Ndugu Charlie. Yale ambayo wamekuwa wakiomba, na yale tumeyaombea, kwa muda mrefu. Dada Ina Bell, ungeweza kusimama, kwa muda kidogo tu? Huyo ni dada Wood... Mdamini wetu hapa kanisani, huyo ni shemeji yake, ambaye amemkubali Yesu kama Mwokozi wake binafsi asubuhi ya leo. . Na ni sala ngapi zimekuwa... Mungu akubariki, Dada Ina Bell. Nadhani nimelitaja jina lako sawa. Hiyo ni kweli? Mungu na akubariki daima, dada mpendwa. Na ikiwa hujawahi kubatizwa katika Jina la Yesu Kristo, nakusihii ufanye hivyo, na umpokee Roho Mtakatifu.

Mungu daima awe pamoja nawe, ambariki mume wako wa thamani pale. Nilikutana naye, siku chache zilizopita. Kama sijakosea, jina lake ni Stanley. Hiyo ni kweli? Stanley. Mungu akubariki, Stanley. Nyumbani ni kutamu, lakini ninaamini kutakuwa kutamu zaidi sasa kuliko hapo awali. Mungu daima awe pamoja nanyi nyote, na—na awape neema Yake na rehema, siku zote za maisha yenu. Na mfuate Bwana. Kuwa kama Ruthu sasa, Ina Bell, shikilia kwenye Hilo. Endeleeni tu kusonga mbele. Wakati mwingine itakuwa vigumu, na njia zitafifia. Lakini, kumbuka, angalia chini tu kuelekea ardhini, kisha angalia juu kuelekea angani, utapata nyayo za Damu ambazo zinafuatisha moja kwa moja hadi huko juu. Yeye ataongoza njia.

93 Sasa, loo, tayari ni adhuhuri, saa sita. Mngali tayari kufanya mstari wa maombi? [Kusanyiko linasema, "Amina." — Mh.]

Billy, wapi, ni aina gani ... Je! Alitoa kadi za maombi? Mimi—mimi kamwe ... Ninaamini aliniambia alitoa maombi ... Vema, ilikuwa ni nini? Mtu fulani aniambie herufi na namba zilikuwa nini. [Mtu fulani anasema, "Huyo hapo anakuja." — Mh.] Nini? [Ndugu Billy Paul anasema, "B."] B. B, moja hadi mia moja? Hamsini hadi mia moja. Vema. B, namba moja. Wao wana ...

Sasa, tuna umati wa watu, kwa hivyo hatuwezi... Tutawafanya wote wasimame, nasi tutawapitisha tu, wakati nikiwaombea.

94 Sasa, ni wangapi hawajawahi kuona mmoja wa mistari ya maombi? Hebu tuone mikono yenu, hamjawahi kuwa katika mmoja wa mikutano yangu, kwenye mstari wa maombi. Loo, jamani! Wengi wenu.

Vema, sasa, tunaweza tu kuwaombea watu, ama tunaweza kuwa na utambuzi, ama tusiwe na mstari wowote wa maombi hata kidogo; waite tu moja kwa moja, katika wasikilizaji. Haijalishi. Roho Mtakatifu yuko hapa. Naam, bwana. Lakini hebu na tusimame kwenye mstari wa maombi.

Namba moja, ni nani aliye na namba moja, kadi ya maombi B? Nam- ... Hamsini. Samahani. Hakuna aliye na moja, bila shaka. Vema. Kadi ya maombi hamsini, ni nani aliye nayo? Njoo huku, bwana. Kadi ya maombi namba mbili ...

Hamsini na moja, hamsini na mbili. Kadi ya maombi hamsini na mbili. Vema. Hamsini na tatu. Hamsini na tatu. Vema. Hamsini na nne.

Njoni huku, papa hapa. Kama uko nyuma, njoo huku, upande *huu*.

Hamsini na moja, hamsini na mbili, hamsini na tatu, hamsini na nne. Ni nani aliye na hamsini na tano, kadi ya maombi hamsini na tano? Yule mama, papa *hapa*. Kadi ya maombi hamsini na sita.

Simama, upande wa ukuta, *pale*, tafadhali.

Hamsini na saba, hamsini na nane, hamsini na tisa, sitini. Sitini na moja, sitini na mbili, sitini na nne, sitini na nne, sitini na tano.

Busty, pita kulia kupitia kwenye marefu hayo papo hapo, ndugu, papo *hapo*. Vema. Geuka moja kwa moja.

Ni wangapi wasio na kadi ya maombi, nawe unataka Bwana akuponye? Inua mkono wako. Vema. Hilo tu ndilo unalopaswa kufanya, amini tu hilo sasa. Amini tu. Vema.

Hamsini na sita. Nilikuwa nayo? Hamsini na saba, hamsini na nane, hamsini na tisa, sitini. Acha wasimame.

Sitini na moja,-mbili, tatu, nne, tano. Acha wasimame. Sitini na sita, sitini na saba, sitini na nane, sitini na tisa, sabini. Acha wasimame.

Sitaki wote wakimbie kwa wakati mmoja, ndiyo sababu ninaita hizo namba, hadi sabini.

Sabini hadi themanini, simama. Njoni huku, upande *huu*, sabini hadi themanini. Vema. Moja, mbili, tatu, nne, tano, sita, saba, nane, tisa. Vema.

Themanini hadi tisini, simameni *hapa*. Doc, wewe wasaidie kule nyuma, tafadhali. Themanini hadi tisini, simameni upande *huu*.

Tisini hadi mia moja, simameni upande *huu*, *hapa*. Vema.

95 Wakati wanapopanga mstari, ningetaka kuliuliza kanisa jambo fulani. Ni wageni wangapi walio hapa, hawajapata kuwa katika mmoja wa mikutano yangu hapo awali? Ni wangapi wenu? Ni wangapi wanaojua ya kwamba hakuna mtu anayeweza kumponya mwingine, si hata daktari? [Kusanyiko linasema, "Amina." — Mh.] La, bwana. Daktari si mponyaji. Yeye husaidia tu maumbile. Mungu ndiye mponyaji. Mnaona? Daktari anaweza kuunganisha mkono, lakini hawezi kuuponya mkono. Daktari anaweza kuondoa kidole tumbo, lakini sio kuponya mahali alipokata. Daktari anaweza kung'oa jino, bali asizuie kutokwa na damu, ama kupaponya. Mungu hana budi kufanya hivyo. Vema.

96 Ni wangapi wanaojua jambo hilo, wakati Yesu alipokuwa hapa duniani, ya kwamba Yeye hakudai kuwa mponyaji? [Kusanyiko linasema, "Amina." — Mh.] Yeye alikuwa Mwanadamu. Yeye alisema, "Si Mimi nikitendaye kazi hizo, bali Baba Yangu akaaye ndani Yangu, Ndiye azitendaye kazi." Hiyo ni kweli? ["Amina."] Ni wangapi wanaojua, wakati alipokuwa hapa, nini, iliyoje ... Alikuwa na huduma ya namna gani wakati alipokuwa hapa? Yeye alifanya yale Baba aliyomwonesha kutenda. Hiyo ni kweli? ["Amina."] Ni wangapi wanaojua, wanaojua jambo hilo? ["Amina."] Yohana Mtakatifu 5:19, Yeye alisema, "Amin, amin, nawaambia, Mwana hawezi kutenda neno Mwenyewe, ila lile ambalo amwona Baba analitenda." Hiyo ni kweli? ["Amina."] "Ndivyo afanyavyo Mwana, vivyo hivyo."

Sasa, basi, je, Yesu Kristo ni yeye yule jana, leo, na hata milele? [Kusanyiko linasema, "Amina." — Mh.] Je! Unaamini jambo hilo, kwa moyo wako wote? ["Amina."] Yeye ni yeye yule jana na hata milele. Je! Unaamini, kwamba, Yesu Kristo kuwa yeye yule jana leo na hata milele, kwamba hiyo inaaminisha Yeye kweli ni yeye yule? ["Amina."] Vema.

Yeye ni yeye yule jinsi gani? Ni yule yule katika kila kanuni. Hiyo ni kweli? [Kusanyiko linasema, "Amina." — Mh.] Yeye ni Mungu yule yule, Mponya yule yule, Mw—Mwokozi yule yule. Yeye ni yeye yule, mtazamo ule ule. Hiyo ni sawa. Hiyo ni kweli? ["Amina."] Sawa sawa. Vema. Basi, kama alikuwa ni yeye yule, na ni yeye yule, Yeye atafanya na kutenda vile vile. Hiyo ni kweli? ["Amina."] Sasa, ni wangapi wanaojua jambo hilo kuwa ni Kweli? ["Amina."]

97 Nitachukua muda kidogo hapa. Ninangojea. Haionekani, kwangu mimi, kana kwamba hao ni watu hamsini wanaosimama pale. (Moja, mbili, tatu, nne, tano, sita, saba, nane, tisa, kumi, kumi na moja, kumi na mbili, kumi na tatu, kumi na nne.) La. Baadhi yao labda walienda nyumbani, mapema. Niliwaona watu fulani wakiondoka kule nyuma. Vema, mstari huu mdogo tu, mfupi. Ni wangapi wangetaka kuwa na hili? Ni wageni wangapi kwangu, katika mstari huo? Inua mkono wako, unayejua sijui chochote juu yako. Inua ninii wangu...mkono wako.

Ni wangapi huko nje, wageni, wanaojua sijui lolote kuwahu? Inua mkono wako, kwamba wewe ni mgonjwa. Vema. Ni wangapi wangetaka kuona mstari wa upambanuzi, ili tuweze kuharakisha na kumaliza? [Kusanyiko linasema, "Amina." — Mh.] Ungetaka ... Sasa, haijalishi. Ninaweza tu kuwaombea, kuwaleta moja kwa moja kwenye mstari. Ama, wanaweza kuketi chini, waende tu na kuketi chini. Haijalishi. Roho Mtakatifu anaweza kuitambua, vile vile tu. Unaamini jambo hilo? ["Amina."]

98 Sasa, basi, kama ndivyo ilivyo, basi nyamazeni tu, kwa muda kidogo tu. Kuchelewa kidogo, kwa hiyo tulia tu, kwa muda kidogo tu. Ninataka kuwaulizeni jambo fulani sasa.

Huenda nikawa kwenye maikrofoni mbaya hapa. Zote mbili ni sawa? Zote mbili zimeunganishwa, sawa, *hii* pia? [Ndugu fulani anasema, "Ndiyo." — Mh.] Vema.

Sasa, nyamazeni tu, kwa muda kidogo. Nitaangalia kwenye mstari huu, nione kama ninamjua mtu ye

yote.

Namjua jamaa huyo anayesimama papo hapo. Sasa, ninamjua Earl. Earl, ninakujua, Earl Colvin. [Ndugu Earl Colvin anasema, "Mimi siko kwenye mstari wa maombi, hata hivyo, Ndugu Bill. Nilimleta rafiki yetu kutoka Jeffersontown." — Mh.] Loo, naam, naam, mtu huyu hapa. Huyu ndiye yule mtu tuliyewinda naye, kule Colorado? ["Labda hamtatutambua, tumepungua sana."] Loo, jamani! Hakika mimi sina. Ninaamini Earl aliniambia ya kwamba ulikuwa mgonjwa sana, nawe umekuja. Sasa, ikiwa huwezi kusimama kwa muda mrefu, hebu mtu ampelekee kiti hapo. Ama, baadhi yao—baadhi yao wanaamka na kumpa kiti papo hapo karibu, itakuwa sawa, maana mtu huyo ni mgonjwa sana, sana. Jamani! Amepoteza karibu pauni mia moja au zaidi, ya uzito. Na—na yeye—yeye ni mgonjwa sana, sana. Sasa hebu acha tu aketi pale. Anza kumshukuru, hapo, ndugu.

99 Sasa hebu niangalie chini. Sasa, Earl alikuwa amesimama tu pamoja naye. Sasa, mtu *huyu*, anayesimama moja kwa moja kule nyuma, akiniangalia, kutoka kote La—LaGrange, Kentucky. Sijui jina lake, bali ni—ni—ninakujua. Na huyo ni Ndugu na Dada Kidd pale. Ninawajua. Na mama huyu, sawa ... Huyu ni Dada Rook? Ama ... [Ndugu Neville anasema, "Dada Hardy." Dada fulani anasema, "Mimi ni Dada Taylor ...?... Pamoja na Hattie." — Mh.] Nikiwa na mwanamke huyu hapa, kutoka Sellersburg, ninaamini, huyo ni kipofu. Hiyo ni kweli? Vema.

Nafikiri hao ni karibu wote, mstarini, ambao kweli nawajua. Loo, naam, huyu hapa rafiki yangu mzuri, Busty Rogers, hapa, kutoka huko chini Milltown. Na huko chini kwenye mstari, nadhani hao wengine ni wageni kwangu. Sasa, hiyo ni mbele za Mungu, nijuavyo mimi, wao ni wageni kwangu.

100 Sasa hebu nione kwenye kusanyiko. Sasa, ninyi—ninyi ambao hatufahamiani, ambao ni wagonjwa, inua mkono wako, na, unajua, una haja moyoni mwako. Inua mkono wako, popote ulipo. Anayejua mimi ... Vema. Sawa. Ni kwa jumla tu, kote, karibu kila mahali.

Sasa, sasa, haitakuumiza, kungoja tu kwa dakika moja ama mbili zaidi. Ninataka kuwaulizeni swali zito. Afadhali nirudi hapa, ili mweze kunisikia. Ninataka tu kuwaulizeni jambo fulani. Sasa, Jumbe hizi ninazohubiri, mnaamini ni Kweli? [Kusanyiko linasema, "Amina." — Mh.] Wewe, hakika, usingekuja hapa kama sivyo.

Sasa, Mungu angefanya kitu kama hicho bila kunipa wazo la kile nilichokuwa nikifanya? Hakika asingeweza. Hakika, asingeweza. Sasa, kama amefanya jambo hilo ...

101 Sasa, ninadai ya kwamba Yesu Kristo hajabadilika. Kifo Chake hakikumbadilisha Yeye; kilimtukuza Yeye. Naye akafufuka, siku ya tatu, na kupaa Juu. Naye alimtuma Roho Mtakatifu, ambaye alikuwa ni Mungu, ni Roho Mtakatifu aliyekuwa juu Yake. Je! Nyote mnaamini jambo hilo? [Kusanyiko linasema, "Amina." — Mh.] Na Yesu, wakati alipokuwa hapa duniani, Yeye alisema, "Kazi nizifanyazo Mimi, ninyi nanyi mtazifanya. Kitambo kidogo, na ulimwengu hautaniona tena." Huo ni utaratibu wa ulimwengu, mwajua, kanisa tu lisiloamini na kadhalika. "Hawataniona tena. Hata hivyo, mtaniona." "Naam," hilo ni Kanisa, mwamini. "Kwa maana mimi ..." "Mimi" ni kiwakilishi nafsi. "Nitakuwa pamoja nanyi, hata ndani yenu, hata ukamilifu wa dahari." Na Kiyunani hapo ni ukamilifu, ambalo linamaanisha, "mwisho wa ulimwengu." "Kuwa pamoja nanyi hata mwisho wa ulimwengu. Na kazi nizifanyazo Mimi ninyi nanyi mtazifanya." Je! Hiyo ni Kweli? ["Amina."]

102 Sasa, tuna Wabaptisti, Wamethodisti, Waprotestanti, na Wakatoliki, na—na hata Wayahudi, wanaoketi hapa asubuhi ya leo. Nasi tuna Church of God, Nazarene, Pilgrim Holiness, Mashahidi wa Yehova, hayo yote madhehebu mbalimbali yamewakilishwa. Ninaangalia kila mahali, nikiwaangalia. Wamethodisti, Walutheri, Wapentekoste, yote mbalimbali, ninapoangalia kote, ninaona watu ninaowajua. Na wote ni wageni kutoka nje ya mji. Maskani ya Branham ni kitu kidogo sana, hapa mjini—mjini, bali ni cha ulimwengu.

103 Sasa, hebu na tuchukue hili tu, na tuwazie kwa makini sana, tuwazie, tuchunguze, tuwe na kicho, na tuilize swali hili. Basi, kama Yeye hajafa, basi mtazamo Wake kwako na kwa wagonjwa ungekuwa ni ule ule leo kama ilivyokuwa jana. Basi Yeye alifanyaje msimamo Wake jana? Huu, "Ninaweza, kama ukiamini." Hiyo ni kweli? [Kusanyiko linasema, "Amina." — Mh.] "Kama unaamini."

Yule mtu akasema, "Bwana, uturehemu." Kasema, "Mwanangu ameshikwa na pepo. Nilimleta kwa wanafunzi wako, nao walikuwa wakipiga makelele na kupiga makelele, na kila kitu."

Akasema, "Ninaweza, kama unaamini. Kama unaamini, ninaweza."

104 Sasa angalia. Yesu alifanyaje? Alikuwa nini, jana? Yeye alihudumuje? Sasa, hili ni kwa mgeni sasa, ninayezungumza naye. Hebu tuone kile alichokuwa, jana. Nichukue tu kama dakika tatu, tutanukuu, sehemu ndogo ndogo.

Wakati huduma Yake ilipoanza kwa mara ya kwanza, kulikuwako na mtu mmoja jina lake Andrea, mvuvi, akaongoka, akamwamini, na akaenda akamchukua ndugu yake, jina lake Simoni. Mnakumbuka

jambo hilo? Alimleta kwa Yesu. Yeye alikuwa mvuvi asiyejua kusoma na kuandika, hata asingeweza kuandika jina lake mwenyewe. Ndipo akaja mbele za Yesu. Ndipo Yesu akamwangukia, na kusema, "Jina lako ni Simoni. Wewe ni mwana wa Yona."

Ni wangapi wanaojua hayo ni Maandiko? Walijua huyo alikuwa ni Masihi, maana Yeye ni ... Mungu aliahidi. Musa aliahidi, ya kwamba, wakati Masihi atakapokuja, Yeye angekuwa ni Nabii. Hiyo ni kweli? [Kusanyiko linasema, "Amina." — Mh.] Nabii-Masihi. Naye akaangalia, na akasema, "Jina lako ni Simoni." Kisha akasema, "Baba yako aliitwa Yona." Naye alijua huyo alikuwa ni Masihi.

105 Yule mwanamke kisimani, hilo ni taifa lingine la watu. Sasa, ni Wayahudi tu na Wasamaria waliompokea. Mataifa, hatukuwa tumeingia bado, kundi la Ruthu. Sasa, yule mwanamke kisimani, ambaye alikuwa Msamaria, alikuja kuteka maji. Yesu alisema, "Nipe maji ninywe." Yeye angefanya nini? Nilizungumza naye, kama tu vile ningezungumza na mtu fulani huko kwenye wasikilizaji. Kasema, "Nipe maji ninywe." Hawakukutana hapo kabla.

Naye akasema, "Mbona, si desturi, tuna ubaguzi hapa." Kama ilivyokuwa huko Kusini, kwa ajili ya marafiki wetu weusi na kadhalika, bali hawana tena. Mungu ashukuriwe, kwa ajili ya jambo hilo. Kwa hiyo akasema ... "Tuna ubaguzi hapa. Mbona, siyo kawaida Kwako. Wewe ni Myahudi." Yesu alikuwa Myahudi. Alikuwa ni Msamaria. Kasema, "Sio kawaida kwa—kwako Wewe kuniomba, mwanamke Msamaria, kitu kama hicho."

Yeye alisema, "Lakini, mwanamke, kama ungalijua ni Nani unayezungumza Naye, ungeniomba Mimi maji."

Hilo lilimsimamisha mwanamke huyo mrembo. Naye akaangalia juu akasema, "Mbona, huna kitu cha kuchotea. Kisima ni kirefu."

Yeye alisema, "Maji ninayotoa ni Uzima wa milele."

Na hatimaye akatambua shida yake ilikuwa ni nini. Ni wangapi wanaojua, wageni, wanaojua shida yake ilikuwa ni nini? Alikuwa na waume watano. Kwa hiyo Yeye alimwambia nini? Akasema, "Nenda, kamwite mumeo uje naye hapa."

Akamwangukia. Akasema, "Sina mume yeyote."

Akasema, "Umesema vema, kwa sababu umekuwa na watano, na yule unayeishi naye sasa si mume wako."

106 Akasema, "Bwana, naona ya kwamba Wewe ni nabii. Sasa, tunajua, Masihi ajapo," (Huyo ni Yesu.) "Masihi ajapo, Yeye atatwambia mambo haya, maana tunajua Yeye atakuwa ndiye Nabii huyo. Tunajua wakati Masihi atakapokuja, Yeye atafanya jambo hili. Lakini Wewe ni nani?"

Yeye alisema, "Mimi Ndiye."

Na juu ya hayo, alikimbilia mjini na kusema, "Njoni, mwone Mtu, aliyeniambia mambo niliyofanya: Haimkini Huyu kuwa ndiye Masihi mwenyewe?"

Kama hiyo ilikuwa ni ishara ya Masihi jana, na ni yeye yule leo, ni jambo lile lile leo. Sasa, hivi ninyi wageni mnaamini jambo hilo? Sasa, hiyo ni kwa ajili yenu katika mstari *hapa*.

107 Sasa, kwao huko ng'ambo, Andiko moja tu, kusudi upate kitu cha kusimama. Ni wangapi wanaoamini ya kwamba Yeye ni Kuhani Mkuu sasa, anayeweza kuguswa na mambo ya udhaifu wetu? Sisi sote ... [Sehemu tupu kwenye kanda — Mh.] ...?...

Baba wa Mbinguni, Yule anayenijua, anayejua, nijuavyo mimi, sijawahi kumuona mtu huyo. Sasa huenda ikawa yeye ameniona na labda naweza kuwa nilimwona, lakini kama tumeonana sijui chochote juu yake. Maana, nimekuwa ulimwenguni kote, wakati mwingine, nikiwaomba wagonjwa na kadhalika, na huenda ni—nilikutana naye mahali fulani, ama kumwona, ama kitu fulani, sijui. Lakini hata hivyo, si—sijui kitu kumhusu. Hiyo ni kweli. Hiyo ni kweli, bwana? Ili tu kwamba watu wajue. Mnaona? Vema. Sasa, mtu huyo anasimama hapa kwa sababu fulani. Sasa yuko wapi huyo jamaa ambaye ni mwindaji, Efferson, ama, kila- ... Vema. Ninataka tu aone jambo hilo. Yuko wapi huyo, Busty Rogers yuko wapi? Amesimama tu pale. Sasa hapa, sasa Busty, unanijua. Bw. Efferson, unajua (Hiyo ni kweli? Efferson? Naam.), Unanijua, tuliwinda pamoja huko Colorado, mimi—mimi ni mtu. [Sehemu tupu kwenye kanda — Mh.]

... Mtu anaogua ugonjwa wa wasiwasi. Hiyo ndiyo shida yake; maana una tezi dume (Hiyo ni kweli.), kuamka usiku, na kadhalika. Umetoka Ohio. Nawe ni mfuasi wa kanisa la Ndugu Sullivan ama unaenda huko. Ninamwona Ndugu Sullivan amesimama hapa. Umekuwa na akina Kidds; huyo ndiye uliyekuja naye. Hiyo ni kweli. Vema, wakati huu unajisikia tofauti sasa. Umekuacha. Sasa, unaweza kwenda nyumbani; imani yako imekuponya. Sasa, Mungu awabariki.

Sasa mnaamini?

108 Sasa sikujui, bwana. Uso wako unaonekana wa kawaida kwangu, lakini sasa, kuhusu kukujua wewe, Mungu Mbinguni anajua, sijui kitu kukuhusu. Sijui una shida gani. Nisingekuwa na njia ya kujua shida yako. Wewe ni mtu tu anayesimama pale. Nawe ulikuwa na kadi ya maombi, kwenye ... ilikuwa na namba. Nawe unaninii tu ... Mvulana huyo alikupa kadi hiyo, nawe uliitwa tu hapa kwenye mstari wa maombi.

Sasa, angalia tu jinsi inavyoibuka. Mnaona, mara hiyo moja tu, hiyo ni ngumu zaidi, hiyo imenifanyia mengi zaidi, mara hiyo moja, kuliko wakati wote ambao nimekuwa nikihubiri asubuhi ya leo. Kitu fulani kikitoka. Mnaona? Kitu fulani kikitoka.

Jamaa mdogo, kwa kweli haupo hapa kwa ajili yako mwenyewe. Uko hapa kwa ajili ya mtu mwingine, na huyo ni m—mtoto. Na mtoto huyo hayupo hapa; ni katika nchi tambarare: Kansas. Ana namna fulani ya vipindi kama kifafa. Hicho ni kifafa, kuna giza juu ya huyo mtoto.

Mna uhusiano fulani, au, wewe ni...na akina Stricker. Si nyote mlia dada, ama kitu kama hicho? Hiyo ni kweli. Unaamini? Ndipo basi hatakuwa na vipindi vingine tena, kama utaamini kwa moyo wako wote. Kama vile ulivyoamini, na iwe hivyo kwa mtoto. Nenda sasa na usitilie shaka.

Sasa unaamini kwa moyo wako wote? Ninyi watu wote? Kumwomba mtu fulani. Omba na umwache Mungu ajalie.

109 Bibi huyo anayeketi pale, akimwomba shangazi huyo, ana kansa; huko chini. Unaamini kwa moyo wako wote, huko nyuma, sivyo? Sikujui. Sijawahi kukuona maishani mwangu. Lakini wakati uliponisikia nikimwambia mtu huyo juu ya jambo alilokuwa akifikiria, juu ya jamaa, hilo lilikujia wewe. Sasa, unaamini kwa moyo wako wote?

Sasa, yeye aligusa nini? Ninataka baadhi yenu ninyi watu, niambieni kile mwanamke huyo alichogusa. Yeye yuko futi ishirini kutoka kwangu yeye hakunigusa mimi, bali alimgusa huyo Kuhani Mkuu. Unaona, Busty? Unaona, bwana? Alimgusa Kristo. Kristo anakuja na kuniambia kile alichokuwa akitaka, sasa anapata alichomba.

Mwanamke, simjui mwanamke huyu. Yeye ni mgeni kwangu. Hiyo ni kweli? Hatufahamiani. Sijapata kumwona maishani mwangu nijuavyo mimi, bali Mungu anamjua. Je! ingekuwa ni Mungu? Ungeamini?

(Sasa, hawa ni wawili, au hawa ni wangapi? Tayari tumekuwa na watatu? Wawili? Wawili? Vema. Sawa.)

Bibi huyo ana kivuli cha mauti. Kuna kivuli cheusi juu yake, ambapo ana kansa. Hiyo ni kweli. Daktari anakwambia ya kwamba ni kansa ya tezi ya limfu. Hiyo ni kweli, inua mkono wako. Umetoka hapa: Iowa. Unaamini? Una, aidha mwana, ama, ni mjukuu, na macho yake yana kasoro, nawe unamwomba. Unaamini Mungu anaweza kuniambia wewe ni nani? Bibi McKee, kisha urudi nyumbani kwako, na uwe mzima. Yesu Kristo anakuponya.

Je! Unaamini kwa moyo wako wote sasa? Sijapata kumwona mwanamke huyo maishani mwangu. Ni kitu gani kinachofanya hivyo?

110 Hebu kidogo tu. Kicho, kwa muda kidogo tu. Ninamtazama moja kwa moja mwanamke mweusi anayeketi huko nyuma kabisa; na hiyo Nuru, mnayoiona kwenye picha hiyo, inaning'inia juu ya mwanamke huyo anayeketi huko nyuma kabisa. Niamini mimi kuwa nabii Wake, dada. Unamwomba mume wako kwenye hatua ya kufa katika Hospitali ya Maveterani; hiyo ni BWANA ASEMA HIVI. Amini kwa moyo wako wote sasa; atapona. Aligusa nini? Yule pale huyo mwanamke, mwanamke mweusi, mwanaume mzungu, kama yule mwanamke kisimani.

Aligusa nini? Yesu yule yule. Yeye si mwanamke yule yule, yule mwanamke mweusi, au, mwanamke Msamaria alivyokuwa; yeye ni mwanamke mwingine. Mimi si Yesu, mtu yule yule; Mimi ni mtu mwingine. Lakini yeye anamwamini Yesu Kristo, kama vile mwanamke alivyokuwa; nami ni mwamini na mtumishi Wake, na Roho yule yule akitenda kazi katika siku hii. Kristo hajafa, Yeye yu hai. Sijapata kumwona wala kumjua maishani mwangu. Sasa, unaona, haikubidi kuwa na kadi ya maombi kuwa hapa. Iweni tu na imani katika Mungu. Hiyo si ni kweli?

Sasa ninajua huyo mwanamke pale, lakini ninajua anachoombea: huyo mpwa. Unaamini (huko kusini), kama utaamini kwa moyo wako wote, atapona.

Na wewe je? Hatufahamiani. Wewe ni kijana tu. Sijapata kukuona maishani mwangu. Unaamini ya kwamba Mungu anaweza kuniambia shida yako ni nini? Je! Akiniambia itakusaidia? Hakika.

Sasa, ninii tu, endeleeni kuamini huko nje. Mnaona?

Shida iko shingoni mwako. Ulipata ajali ya gari. Unashuka kutoka kaskazini. Uko karibu na Bedford,

Indiana. Hiyo ni kweli. Hiyo ni kweli? Ndipo u—unaamini shingo yako itakuwa sawa? Kama unavyoamini, na iwe kwako. Rudi nyumbani na kumpa Mungu sifa. Na uponywe.

U hali gani, bwana? Unaamini ya kwamba Mungu anaweza kunifunulia shida yako? Unaugua ugonjwa wa—wa wasiwasi; ilikufanya uwe na ugonjwa wa utumbo, utumbo mpana, utumbo. Wewe kweli unatoka California. Hiyo ni kweli. Unaamini Mungu anakujua wewe ni nani? Bw. Murray? Vema, umekwisha sasa. Rudi nyumbani kwako; mwamini Yeye kwa moyo wako wote.

Je! Sisi hatufahamiani? Sikujui, na Mungu ... Sikujui wewe wala hunijui. Sisi hatufahamiani, sivyo? Kama Mungu atanifunulia jambo fulani kukuhusu wewe, je! Utaniamini mimi kuwa nabii Wake?

Je! Ninyi wengine mtaamini? Mimi ... Inanifanya kuwa mnyonge sana, mnyonge sana sasa, mnaona. Amini tu sasa. Mimi ninaninii tu ... Upako uko hapa. Mnajua hilo, sivyo? Mna—mnajua ya kwamba iko—iko hapa, mnaona. Roho Mtakatifu yuko hapa sasa kama unaweza tu ... Ninakuwa mdhaifu sana hata ni vigumu kuwaona huko nje tena. Mnaona? Ninyi ... Kama kisa kimoja kilimfanya Yesu kudhoofika, visa saba ama nane, kumi hapa, ambavyo tumekuwa navyo, hapa, kupitia kwa wasikilizaji? Vitano au sita au saba hapa jukwaani pamoja na vitatu, au vinne, au vitano, huko nje. Mnaona? Imenifikisha tu mahali ambapo ni vigumu kuona tena. Inaonekana kama kwamba umati wote unakuwa kama maziwa. Laiti mngelitambua tu huo ni uzito wa Roho Mtakatifu akiingia. Hiyo ndiyo Nuru hiyo, pale, ikitanda juu ya jengo. Mnaona, ni, Yeye anakuingiza katika kundi, mahali fulani.

Sasa, kwa kuwa mwanamke huyu amesimama hapa, kwenu katika mstari wa maombi sasa: Kama Mungu atafunua (Hapa, ninainua mikono yangu juu, sijawahi kumwona mwanamke huyu, sijui kitu juu yake), kama Mungu atafunua. hasa, hebu, kile alichofanya, ama kile alichu, ama, vema, kitu kingine juu yake, je! ninyi nyote mtaamini, basi, ya kwamba, kwamba, Mungu hufanya hivyo? Mtaamini? Na unaweza—unaweza kukubali? Utaamini ya kwamba utaishi sasa? Waweza ... Bila shaka ninajua shida yako, ninajua shida yako, yako, haijafichwa. Unaona? Mungu hufunua mambo hayo, bali kama utaamini tu.

Sasa, nitapitia na kuwawekea mikono maana ninakuwa mdhaifu sana. Nami ninajua katika muda kidogo, vema, ni—nisingeweza kuona tena, mnaona.

Sasa, unaamini kwa moyo wako wote. Sasa kumbukeni, si mimi. Kila mtu anajua jambo hilo. Ni Roho Mtakatifu. A-ha. Sasa, kama ninaweza tu kuishika roho ya mwanamke huyu. Hilo ndilo jambo lile lile alilofanya Yesu. Akijaribu kuishika roho yake, Yeye alisema, "Nipe maji ninywe."

Huyu hapa mwanamume na mwanamke, kama tu ilivyokuwa pale. Sasa, wewe ni mwanamke kijana, mdogo sana kuliko mimi. Sasa, labda, labda mwanamke huyu alikuwa mdogo kuliko Yesu. Alikuwa na umri wa kama miaka thelathini na mitatu; na labda hakuwa na umri wa miaka kumi na minane ama ishirini, msichana tu. Na yeye—yeye—yeye alikuwa vigumu kujua la kusema ila wakati alipozungumza naye alisema, "Nipe maji ninywe."

Sasa Baba alikuwa amemtuma Samaria. Alikuwa akienda zake Yeriko, bali alizunguka Samaria; hiyo ni juu ya mlima. Kwa nini alifanya hivyo? Yeye alisema alikuwa na haja ya kupitia. Baba alimtuma kule. Vema, Yeye alikuja tu na kuketi chini, na akawatuma wanafunzi mjini wapate chakula. Na maskini msichana huyu mrembo akaja kuchota maji, na hapana budi Baba alisema, "Ninamwita."

Yeye alisema, "Mwanamke, nipe maji ninywe." Ndipo mazungumzo yakaanza. Sasa, jambo lile lile hapa.

Je! Uliweka mkono wako kwenye koti langu? Mmoja wenu? Hapana bwana. Mungu Mbinguni anajua Kitu fulani kilinigusa wakati huo, wakati ... Nilidhani ilikuwa ni Billy akiniambia niondoke. Mnaona. Mi—mi—mikono yangu, Mungu anajua hiyo ni kweli. Kitu fulani kilinigusa namna hiyo nami nikafikiri ni Billy akiniambia, "Nenda zako." Mnaona, ni—wakati unapokuwa namna hii, ni vigumu kwako kujua, hujui wakati wa kusimama ama la kufanya. Mnaona? Karibu tu umejisahau. Nilikuwa ninazungumzia nini? Yule mwanamke kisimani.

Na ndipo baada ya Yeye kuona mahali shida yake ilipokuwa, Naye akasema, "Nenda, kamlete mumeo."

Akasema, "Sina." Naye akamwambia, akasema alikuwa na watano.

Ndipo akasema, "Naona ya kwamba Wewe ni nabii. Ninajua Masihi ajapo, Yeye atatuambia mambo haya."

Sasa je! Huyu angekuwa Masihi yule yule leo, kama ningeweza kuwaambia jambo fulani, jambo fulani baya? Kama Mungu hatakusaidia, utakufa. Una saratani. Sasa, unaamini Mungu anaweza kuniambia hiyo saratani iko wapi? Iko tumboni. Unaamini Mungu anakujua wewe ni nani? Unaamini Mungu anajua unakotoka? Umetoka Illinois. Wewe ni—jina lako ni Bibi Johnson. Rudi upate kuishi. Yesu Kristo anakuponya. Unaamini kwa moyo wako wote? Ninii tu ... Hebu aishi ...?... Kuna sababu ya mimi kukwambia



uishi.

Baba wa Mbinguni, katika Jina la Bwana Yesu, ninaweka mikono yangu juu ya mwanamke huyu sasa; upako wa Roho Mtakatifu upo hapa. Mponye, Bwana, katika Jina la Kristo, Yesu.

Mungu mpendwa, juu ya ndugu yetu wa thamani, ambaye Wewe uliyaokoa maisha yake huko nyuma, katika Agosti, Ee Mungu mwenye rehema, njoo kwake sasa, wakati Roho Mtakatifu anaipaka mafuta mioyo yetu. Ninajua kujaribiwa kwa ndugu yangu. Mponye, Bwana, na umpe afya...?...

Ulikuwa na mshtuko wa moyo, una ugonjwa wa kisukari; najua unaugua, hata hivyo, hiyo ni...?...

Baba yetu wa Mbinguni, mtu huyu ni ...?... Hana budi kukupata ama afe. Yeye anapenda kwenda hospitalini ...?... Msamehe dhambi zake na uponye mwili wake katika Jina la Yesu Kristo na aishi. Nenda nyumbani, nenda.

Vema, hapa, ninyi nyote mchukueni ndugu huyu nyumbani.

Mungu wetu wa thamani, katika Jina la Yesu Kristo, mikono yangu juu yake wakati upako wa Roho Mtakatifu umekaribia. Hebu watu watambue. Hebu na aponywe.

Baba Mungu, ninapoweka mikono yangu (mikono yangu, mwili wangu haustahili, umeharibika, umeharibika na ni mwovu; bali Roho Mtakatifu yu juu yangu sasa), jalia nguvu zinazoweza kutambua mawazo ya moyo zimjali mwanamke huyu na kumponya mwili, katika Jina la Yesu.

Mungu mpenzi, nikimjua ndugu yangu na hali yake, nikijua ya kwamba kizuizi hiki cha kunena ... [Sehemu tupu kwenye kanda — Mh.]

Ee Mungu, juu ya kijana wanamume huyu, akipigana vita vizuri vya imani, akisimama Uweponi mwa Yehova-Yire, Dhabihu ya Bwana iliyotolewa, jalia nguvu zilizomfufua Yesu kutoka kaburini, zimguse sasa hivi. Mpe shauku ya moyo wake, katika Jina la Yesu Kristo. Amina.

Bwana Yesu, juu ya dada yangu ninaweka mikono yangu. Katika Jina la Yesu Kristo, jalia macho hayo yaponywe. Jalia mateso yake—yake yaondoke mwilini mwake, katika Jina la Yesu Kristo. Amina.

Baba yetu wa Mbinguni, kwa ajili ya Dada yangu mdogo Kidd, ninaomba ya kwamba utashinda ndani yake, na umpe nguvu katika uzee wake kama ulivyompa Naomi. Bwana, jalia angali atumiwe kwa ajili ya utukufu Wako. Tujalie, Baba, katika Jina la Yesu Kristo.

Ndipo kwa Ndugu Kidd, Bwana, mauti hayo yalimgusa, bali Uzima ulimrudisha. Mungu, ninaomba ya kwamba utamtia nguvu. Yeye amepita wakati wake aliopewa. Lakini Wewe ni Mungu, nawe utafanya jambo hili kwa utukufu Wako kama ulivyonihi hospitalini. Sasa, mpe nguvu kwa ajili ya ushuhuda. Jalia ushuhuda wake usikike kote katika jimbo la Ohio, kote ulimwenguni. [Sehemu tupu kwenye kanda — Mh.]

Kwamba Yesu ananiponya sasa.  
Nitamchukua kwa Neno Lake ...



[www.messagehub.info](http://www.messagehub.info)

Mahubiri Na  
**William Marrion Branham**  
"... katika siku za sauti ..." Ufu. 10:7